


# CHANGAMOTO YA MSALABA

Je, msalaba bado ndio kiini cha Ukristo leo?

Miki Hardy

# Changamoto ya Msalaba

na Miki Hardy

Hakimiliki © 2019 na Church Team Ministries International

**Changamoto ya Msalaba** na Miki Hardy

Imechapishwa na Church Team Ministries International

Toleo la kwanza: Juni 2019

Hiki kitabu kimetolewa chini ya leseni ya Creative Commons Attribution-NonCommercial-NoDerivatives 4.0 International License.

Ili kuiona nakala ya leseni hii, tembelea https://creativecommons.org/licenses/by-nc-nd/4.0/

Pata makala za bure za CTMI kwa njia ya ki-eletroniki katika www.ctmi.org
Tumia mafundisho haya kwa uadilifu.

Vifungu vya Biblia vimetolewa katika Biblia, Swahili – Union Version, 1962. Haki zote zimehifadhiwa.

ISBN 978-99949-941-4-4

# Yaliyomo

Utangulizi ........ 5
I. Wokovu na Msalaba ........ 8
II. Ubatizo na Msalaba ........ 10
III. Meza ya Bwana na Msalaba ........ 12
IV. Maombi na Msalaba ........ 15
V. Toba na Msalaba ........ 19
VI. Msamaha na Msalaba ........ 24
VII. Neema na Msalaba ........ 30
VIII. Majaribu na Msalaba ........ 34
IX. Ushindi na Msalaba ........ 36
X. Mateso na Msalaba ........ 39
XI. Imani na Msalaba ........ 43
XII. Ukomavu wa kiroho na Msalaba ........ 46
XIII. Uhuru na Msalaba ........ 52
XIV. Msalaba na Uhai wa Kristo Ndani Yetu ........ 55
Wokovu katika Yesu Kristo ........ 58

# Utangulizi

Tunapoliangalia Kanisa la Kwanza katika kitabu cha Matendo ya Mitume tunaona kanisa lenye nguvu, umoja, lililokuwa hai na lililojitenga na dunia. Ni wazi kwamba ujumbe wa injili uliohubiriwa wakati ule ulikuwa na nguvu. Ulileta toba ya kweli, kujitoa kwa dhati, kusameheana kwa kweli, umoja wa wazi na imani isiyopungua neno. Kanisa la Kwanza lilikuwa na safari ya dhati kuuelekea ukomavu wa kiroho, na kila Mkristo alielewa waziwazi ya kwamba maisha ya Ukristo yalimaanisha kuutoa uhai. Walikuwa tayari kujifananisha na Kristo, katika mateso yake, mauti yake na kufufuliwa kwake.

Mtume Paulo alipokea moja kwa moja kutoka kwa Yesu Kristo mwenyewe utimilifu wa ufunuo wa injili: Yesu Kristo, naye amesulubiwa, kama anavyoeleza katika Wagalatia 1:11-12, *“Kwa maana, ndugu zangu, injili hiyo niliyowahubiri, nawajulisha ya kuwa siyo ya namna ya kibinadamu. Kwa kuwa sikuipokea kwa mwanadamu wala sikufundishwa na mwanadamu, bali kwa ufunuo wa Yesu Kristo.”* Yesu Kristo aliyesulubiwa ndio ujumbe wa msingi wa Agano Jipya.

Maadam ujumbe wa msalaba uliendelea kuhubiriwa, Wakristo wa kanisa la kwanza walibaki imara na wenye nguvu; msingi wao ukiwa imara katika Kristo. Walienenda katika ushindi, utakatifu na imani. Lakini mara tu ujumbe huo ulipochanganywa na kughoshiwa, imani yao ililegea na wakaacha kuenenda katika njia za Bwana, kama tunavyoona waziwazi katika nyaraka kwa Wagalatia, Waebrania na Wakorintho.

Mwandishi wa Waebrania anaelezea bidii na hali ya kujitoa waliyokuwa nayo Wakristo wa Kiyahudi mara walipoupokea ujumbe halisi wa injili. Walikuwa tayari kustahimili aibu nyingi, mateso na adha, na walishiriki kwa furaha vitu vyao vyote (Waebrania 10:32-34). Hata hivyo baadaye, moto ulipoanza kupoa mioyoni mwao imani yao ilipungua nguvu na tunaona jinsi tabia yao ilivyobadilika walipoanza kujiweka tena chini ya matakwa ya Torati ya Musa.

Makanisa mengi leo yanaona ni heri kupuuza kuhubiriwa kwa msalaba na badala yake wanahubiri jumbe ambazo badala ya kuivuta mioyo ya Wakristo

kumwandama Yesu na kutengwa na dunia zinabaki kuwatimizia tamaa zao za kimwili katika kuyaandamia mambo ya ulimwengu huu, ingawa Biblia inayaelezea haya mambo kuwa ni ya muda tu.

Hii ndiyo sababu tunahitajika kuelewa kikamilifu maana ya kile kilichofanyika msalabani, na umuhimu wake katika fundisho zima la Ukristo. Kisha tutaanza kuelewa ya kwamba msalaba wa Yesu Kristo ndio msingi wa kweli wa Ukristo, na kwamba unahusika katika kila eneo la fundisho lake. Kile kilichofanyika msalabani ni lazima kiwe halisi maishani mwetu, na si tukio lililotokea miaka elfu mbili iliyopita tu.

*"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena; kwa kuwa yeye aliyekufa amehesabiwa haki mbali na dhambi. Lakini tukiwa tulikufa pamoja na Kristo, twaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye; tukijua ya kuwa Kristo akiisha kufufuka katika wafu hafi tena, wala mauti haimtawali tena. Maana kwa kule kufa kwake, aliifia dhambi mara moja tu; lakini kwa kule kuishi kwake, amwishia Mungu. Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu."* (Warumi 6:3-11).

Tunapolisoma hili andiko kwa umakini, tunaelewa ni nini hasa kilichofanyika pindi Yesu alipokufa na kufufuka. Kutokana na upendo wake mkuu na shauku aliyokuwa nayo ya kumuokoa mwanadamu kutoka katika hukumu ya dhambi, Mungu, Baba yetu, aliwajumuisha wanadamu wote katika dhabihu yake kamilifu. Mtume Paulo anathibitisha kwamba sote tulikufa, tukazikwa, na kufufuliwa pamoja na Kristo. Hili linamaanisha ya kwamba 'utu wetu wa kale' (asili yetu iliyokuwa haijakombolewa) umesulubiwa pamoja na Kristo, ili tuenende katika upya wa uzima, tukiwa huru mbali na dhambi na tukiuelekea utakatifu. Je! haistajabishi kuona kwamba mtu mmoja (Yesu) alikufa kwa ajili ya wote ili kwa njia ya mauti yake, wanadamu wote wahesabiwe haki? (Warumi 5:18).

Paulo anasisitiza hili kwa kusema ya kwamba katika Yesu, Mungu amefanya njia, *"...ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo..."* (Waefeso 1:4). Kipawa cha bure cha wokovu kilichoandaliwa tangu kabla ya mwanzo wa nyakati sasa kimekuwa halisi kwa njia ya dhabihu ya Yesu msalabani. Yesu ndiye kipawa cha Mungu na ndiye udhihirisho wa neema yake kwa wanadamu wote. *"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani..."* (Waefeso 2:8). Katika sura iyo hiyo, Paulo anasema pia kwamba tuna kila kitu (kihusucho utakatifu) katika Yesu, kwa kuwa tulikuwa wafu kutokana na dhambi zetu bali sasa tumefanywa hai pamoja naye. Anaendelea kusema ya kuwa Mungu alituketisha *"... pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu..."* (Waefeso 2:6). Huu ufunuo ndio unaotupatia imani inayotuwezesha kuishi maisha matakatifu na yenye ushindi.

Tunawezaje basi, kulielewa hili, na bado tuendelee kuishi maisha yetu jinsi tunavyotaka, kwa kuzifuata tamaa za miili yetu? Ndiyo, ni kweli ya kwamba Yesu alifanya kila lililohitajika msalabani ili sisi tuupokee urithi wetu kamili na ili tuenende kwa ushindi dhidi ya dhambi, lakini hili halitawezekana hadi tujitwike msalaba wetu (Mathayo 16:24). Kama Paulo anavyothibitisha: *"Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulibisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake."* (Wagalatia 5:24).

Yesu mwenyewe alisema waziwazi, *"Wala mtu asiyechukua msalaba wake akanifuata, hanistahili."* (Mathayo 10:38). Je, jambo hili linaweza kuwa wazi zaidi ya lilivyoelezwa hapa? Mtume Paulo alilielewa hili kikamilifu, na ndio sababu akamhubiri, *"...Yesu Kristo, naye amesulibiwa"* (1 Wakorintho 2:2) na kuzungumza juu ya Mkristo kuyafananisha maisha yake na mateso, kifo na kufufuliwa kwake Yesu.

Ujumbe huu ndio msingi wa maisha ya Ukristo na hatuwezi kutarajia kuenenda katika ushindi ikiwa tutapuuza wito huu wa kuyafananisha maisha yetu na Kristo kila siku. Huu ndio ujumbe wa msalaba, ujumbe rahisi, lakini wenye nguvu.

## Sura ya I

# Wokovu na Msalaba

Jambo la kwanza tunalopaswa kufahamu ni kwamba wokovu hupatikana *“... kwa imani [...] kwa njia ya imani…”* (Waefeso 2:8).

## Wokovu, uthibitisho wa upendo wa Mungu

Ufunguo wa wokovu wetu ni mauti ya Yesu msalabani. Tunapoisikia injili ikihubiriwa Roho Mtakatifu hutuhakikisha juu ya dhambi zetu. Tunatambua ya kwamba asili yetu ya dhambi, ambayo ni ya kila mwanadamu, hututenga mbali na Mungu, na ya kwamba ilimpasa Yesu kuteswa na kufa msalabani ili atukomboe. Roho Mtakatifu hutuongoza kujinyenyekeza, kutubu na kuutafuta msamaha wa Mungu tunapoufahamu upendo wake kwetu, kwa kumpokea Yesu Kristo kama Mwokozi wetu. Kisha Roho Mtakatifu huishuhudia mioyo yetu ya kuwa tumekuwa watoto wa Mungu (Warumi 8:16).

Dhabihu ya Yesu msalabani ni uthibitisho wa upendo wa Baba yetu wa mbinguni usiokuwa na kifani na ulio kamili, kwa wanadamu wote: *“...kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.”* (Warumi 5:8).

Mtume Yohana anaandika ya kwamba, *“...Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.”* (Yohana 3:16). Yesu alienda msalabani bila kusita ili kuimwaga damu yake kwa ajili ya kuutimiza mpango wa kipekee wa Mungu wa wokovu kwa wanadamu. Akajinyenyekeza kwa kuuchukua mfano wa mwanadamu na, katika ubinadamu wake, akaishinda dhambi.

Ukuu usiokuwa na kifani wa upendo wa Mungu na mpango wake wa wokovu kwa mwanadamu unadhihirika katika kitabu cha Isaya sura ya 53. Nabii anaelezea kwa kina mateso ambayo ilibidi Kristo ayapate. Mungu aliweka uovu wetu wote juu ya Mwanawe na adhabu ya amani yetu ilimwangukia. Ulikuwa ni mpango wa Mungu kumvunja Kristo kwa njia ya mateso

yaliyompata kusudi azibebe huzuni zetu. Alilipa gharama msalabani ili sisi tukombolewe kutokana na dhambi zetu zinazotutenga na Baba.

Paulo anazungumzia jinsi Yesu alivyofanyika *“...laana kwa ajili yetu.”* Torati ya Musa, iliyofanyika kuwa laana kwa mwanadamu (kwa kuwa iliifunua hali yake ya dhambi, na hivyo kumhukumu) ilifutwa na dhabihu ya Yesu msalabani alipoitwaa laana juu ya nafsi yake (Wagalatia 3:13). Mahali pengine, anaelezea ya kwamba, *“Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.”* (2 Wakorintho 5:21). Yesu alichukua juu ya nafsi yake hukumu tuliyostahili kwa ajili ya dhambi zetu.

## Toba na imani: funguo za wokovu

Ili kupokea msamaha wa dhambi, wokovu na karama ya uzima wa milele, tunachohitajika kufanya ni rahisi: ni kutubu, kumkiri Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu, kukubali alichofanya msalabani na kumpokea kama Bwana na Mwokozi wetu.

Kuna mifano kadhaa ya kuokoka katika kitabu cha Matendo ya Mitume. Katika sura ya 2 msitari wa 37, Petro anauhubiria umati mkubwa wa Wayahudi siku ya Pentekoste kuhusu wokovu kwa njia ya Yesu Kristo. *“Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu?”* Wengi waliuhisi upendo wa Mungu kwao na watu elfu tatu wakatubu na kumgeukia Kristo siku hiyo. (Matendo 2:41).

Katika Matendo 8:26-38, tunasoma kisa kingine: towashi wa Kushi alikuwa akisafiri kwenye gari lake, na akawa anasoma, katika kitabu cha Isaya, kifungu kinachozungumzia mtu aliyejitoa nafsi yake kuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi za wanadamu. Malaika wa Bwana alimuongoza Filipo hadi kwake na akaweza kumueleza ya kuwa yale maneno yalimzungumzia Kristo. Alimshirikisha habari njema za kifo cha Yesu msalabani na kufufuka kwake na, aliposikia, yule towashi alitubu, akaokoka na kubatizwa na Filipo kwenye maji yaliyokuwa karibu.

Mtume Paulo anatufahamisha ya kwamba injili, ambayo msingi wake ni katika kifo, kuzikwa na kufufuka kwake Yesu (1 Wakorintho 15:1-4), *“...ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye...”* (Warumi 1:16). Anasema waziwazi ya kwamba, *“...Maana msingi mwingine hakuna mtu*

*awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo."* (1 Wakorintho 3:11)

### Msalaba na wokovu: havitenganishiki

Hivyo basi, msalaba wa Yesu Kristo ndio msingi wa wokovu wetu. Yesu angalikuja tu duniani pasipo kufa msalabani na kufufuka, hakuna mtu ambaye angeokolewa. Pasingekuwepo na dhabihu kamili, wala damu iliyomwagika ya Kondoo wa Mungu asiyekuwa na doa, na kwa sababu hiyo pasingekuwepo na msamaha kwa ajili ya dhambi zetu.

## Sura ya II

# Ubatizo na Msalaba

### Ubatizo sio ibada wala si lazima kwa ajili ya wokovu

Kwa bahati mbaya katika makanisa mengi leo, ubatizo wa maji umekuwa ni utaratibu tu wa kidini au hatua ya lazima. Mara nyingi Wakristo hawaelewi kikamilifu ya kwamba uamuzi wa kubatizwa unapaswa kuashiria uamuzi wa dhati wa kuyaishi maisha yao yaliyobaki hapa duniani katika kumtii Bwana. Wakristo mara nyingi hufundishwa tu kwamba ubatizo ni hatua ya pili baada ya kuokoka. Wanahimizwa kwa maneno kama vile, 'Kwa vile umeokoka unapaswa sasa ubatizwe', pasipo kuelezwa kikamilifu gharama halisi ya kumfuata Yesu. Matokeo yake, ubatizo wa maji unakuwa ni tendo la kidini tu lisilokuwa na udhati wa kuyafananisha maisha ya mhusika na Kristo.

Wazo lingine lililopo kanisani leo hii linaenda mbali zaidi na kusema ya kuwa ikiwa mtu amezaliwa mara ya pili lakini hajabatizwa, atakuwa hajaokoka. Lakini tunaona katika Warumi 10:9, *"Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka."* Kwa kuwa ubatizo hufuatia baada ya mtu kuwa ameokoka, ni wazi katika kifungu hiki ya kwamba mtu aliyefariki baada ya kuokoka ila hajabatizwa bado atarithi uzima wa milele.

## Kujifananisha na Kristo

*"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Warumi 6:3-4). Katika mistari ya awali Mtume Paulo anaeleza ya kwamba ikiwa tumeifia dhambi, hatuwezi kuendelea kuishi katika dhambi. Hili linawezekana kwetu kwa sababu kama vile Yesu alivyofufuliwa kutoka kwa wafu, sisi pia tutaweza kuishi katika upya wa uzima katika Kristo.

Katika ubatizo, Mkristo huzamishwa kabisa majini, jambo linaloashiria kuifia nafsi. Kisha hutoka majini, ikiwa ni ishara ya kufufuliwa katika upya wa uzima, na sasa anakuwa ameitwa kuishi maisha matakatifu katika Yesu. Mkristo basi anapaswa kuelewa uzito wa uamuzi wake wa kujifananisha na mateso na kifo cha Kristo kabla hajabatizwa.

## Uamuzi wa kuifia nafsi

Yesu pia alizungumzia ubatizo alipokuwa akijibu swali kutoka kwa Yakobo na Yohana, alipowaambia, *"Mwaweza kunywea kikombe ninyweacho mimi, au kubatizwa ubatizo nibatizwao mimi? [...] Kikombe ninyweacho mimi mtakinywea, na ubatizo nibatizwao mimi mtabatizwa; lakini habari ya kuketi mkono wangu wa kuume au mkono wangu wa kushoto si langu kuwapa, ila wao watapewa waliowekewa tayari."* (Marko 10:38-40).

Tunaona katika kifungu hiki cha Maandiko ya kwamba Yesu alikuwa anawauliza wanafunzi wake kama walikuwa tayari kubatizwa ubatizo ambao yeye mwenyewe angebatizwa. Ni kwa nini aliwauliza swali hili ilhali tayari alikuwa amebatizwa majini na Yohana Mbatizaji? Bila shaka alikuwa akizungumzia mateso na kifo aliyokuwa akiyaendea msalabani. Ni kana kwamba alikuwa akiwauliza: 'Mtakuwa tayari kuuchukua msalaba wenu?' Katika hali halisi, Yesu alikuwa akiwaonyesha uhusiano uliopo kati ya ubatizo na msalaba ambao kila Mkristo ameitwa kuubeba.

Hii, basi, ndiyo maana ya Mathayo 16:24, *"...Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate."* Ubatizo ni tendo linaloashiria utayari wa Mkristo wa kuutoa uhai wake, kujikana nafsi na kuuchukua msalaba wake mwenyewe, ili kumfuata Yesu. Ni uamuzi

makini wa hadharani wa kuyaishi maisha mapya: kujazwa uhai wa Kristo ili tumtumikie kikamilifu.

Ubatizo wenyewe haumbadilishi Mkristo, bali unampa changamoto ya kuutoa uhai wake ili ayabebe maisha ya Kristo, na kumuishia. Hii ndiyo maana ni muhimu kuelewa ubatizo katika msingi wa ufunuo wa msalaba wa Yesu.

Ni wazi kwamba ikiwa Mkristo hayuko tayari kuifia nafsi yake, hana haja ya kubatizwa! Na katika hili tunaelewa ni kwa nini Yesu aliwaambia wanafunzi wake ya kwamba ikiwa mtu atastahili kumfuata, ni lazima ajikane mwenyewe na kuuchukua msalaba wake. Kwa maana hiyo, ubatizo unachukua maana mpya kabisa tunapotambua jinsi ulivyofungamana na msalaba wa Yesu Kristo.

## Sura ya III

# Meza ya Bwana na Msalaba

Katika sura iliyotangulia tumeangalia maana ya ubatizo wa maji. Je, ubatizo wa maji na Meza ya Bwana vina uhusiano gani? Tumeona tayari ya kwamba ubatizo ni uamuzi wa hadharani wa kuyafananisha maisha yetu na Kristo. Kuishiriki Meza ya Bwana ni uthibitisho wa huo uamuzi na yote mawili yanahusika na ujumbe wa msalaba kama alivyofundisha Yesu.

Kwanza kabisa, Meza ya Bwana ni ukumbusho wa upendo wa Kristo. Mkate hutukumbusha mateso aliyoyapata pale mwili wake ulipovunjwa, na kikombe hutukumbusha damu yake iliyomwagika msalabani.

Tunaposoma 1 Wakorintho 11:20-22, tunaona ya kwamba Wakristo wa Kanisa la Kwanza waliishiriki Meza ya Bwana mara kwa mara, na hili mara nyingi lilifanyika walipokutana majumbani mwao. Tunamuona hata Mtume Paulo akiwakemea Wakorintho kwa kutoichukulia Meza ya Bwana kwa umakini uliostahili kwani kuna hata nyakati baadhi yao walikunywa hadi kulewa humo.

## Ni wakati wa kujipambanua

Walipokuwa wakiishiriki Meza ya Bwana, Wakristo wa kwanza walikumbushwa uamuzi wao wa kuyafananisha maisha yao na Bwana, kwani ni jambo alilowaagiza kufanya (1 Wakorintho 11:24). Kwa jinsi iyo hiyo, Meza ya Bwana ni wakati wa sisi kujichunguza na kuitafakari hali yetu ya kiroho, kujitoa kwetu na utumishi wetu kwa Bwana; ni wakati wa kujiuliza ikiwa tumepoteza maono yetu ya kuyafananisha maisha yetu na Kristo. Je, mioyo yetu iko sawa kati yetu na Mungu na binadamu wenzetu? Huu ni wakati pia ambapo tunaweza kuhisi kuhukumiwa kwa ajili ya dhambi zetu, tukatubu na kuipokea neema yake kabla ya kuendelea na mbio zetu. Vile vile, ni wakati pia wa kusameheana kwani tumeitwa tuwe na amani na watu wote. Hii ndiyo namna tunavyopaswa kuishiriki Meza ya Bwana.

Jambo la kusikitisha ni kwamba kwa Wakristo wengi jambo hili limebaki kuwa ni utaratibu wa kidini na limepoteza maana halisi iliyokuwepo enzi za Kanisa la Kwanza. Na hakika, katika makanisa mengi leo, msalaba hauna nafasi tena katika Meza ya Bwana.

Kwa hivyo, je! tunapaswa kuishiriki Meza ya Bwana majumbani mwetu mara kwa mara na familia zetu, na tunapokutana kama jamii ya waaminio? Jibu langu ni, Kwa nini tusishiriki? Bila shaka jambo hili litatusaidia katika kumkaribia Bwana zaidi.

## Kukumbushwa kuuchukua msalaba wetu

Tukirejea msitari uliotajwa hapo awali katika Marko 10:30, tunaona Yesu aliwauliza wanafunzi wake ikiwa walikuwa tayari kukinywea kikombe ambacho yeye angekinywea. Kwa mara nyingine tena, hapa anazungumzia mateso na kifo chake msalabani. Kimsingi, anawauliza, Je! mtakuwa tayari kuuchukua msalaba wenu na kunifuata? Mtakuwa tayari kuyafananisha maisha yenu na mateso na mauti yangu; kuyapoteza maisha yenu ili myapate maisha yangu? Changamoto iliyopo hapa ni sawa na ile iliyopo pale alipowauliza ikiwa walikuwa tayari kubatizwa kwa ubatizo ule ule ambao Yeye angebatizwa nao.

Hiyo ndiyo sababu Yesu akawaambia, *"...Amin, amin, nawaambieni, Msipoula mwili wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu."* Hapa Yesu hakuwa akizungumzia kuula mwili wake

wa damu na nyama bali alinena juu ya lile ambalo lingetimilika katika maisha ya kila aaminiye kupitia mwili wake uliovunjwa na damu yake iliyomwagika msalabani.

Mkate tunaoumega tunapoishiriki Meza ya Bwana ni mfano wa mwili wake uliovunjwa kwa ajili yetu kwa njia ya kuteswa kwake. Yesu aliteseka katika mwili wake, alipigwa na kuumizwa, na tunapoula mkate tunathibitisha uamuzi wetu wa kuyafananisha maisha yetu na mateso yake. Kwa maneno mengine, tunadhihirisha utayari wetu wa kuteseka pamoja naye kama Mtume Paulo anavyosema katika Wafilipi 1:29, *“Maana mmepewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, ila na kuteswa kwa ajili yake”.*

Yesu anatuhakikishia ya kwamba ikiwa hatutaula mwili wake au kuinywa damu yake, kwa maana nyingine, ikiwa hatutaki kuyafafanisha maisha yetu na mateso na mauti yake, hatuwezi kuyashiriki maisha yake ya ufufuo. Kikombe kinaashiria kifo chake na kipawa cha uzima wake, na tunapoishiriki Meza ya Bwana, tunaitangaza upya shauku yetu ya kujikana wenyewe na kuutoa uhai wetu, ili tuubebe uzima wake. Paulo anaeleza hili waziwazi katika Wagalatia 2:20, *“Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu...”*

## Kabla au baada ya ubatizo?

Baadhi ya Wakristo hujiuliza kama wana haki ya kushiriki Meza ya Bwana kabla ya kubatizwa. Siamini kuwa ni suala la kuwa na haki au la, bali ni iwapo tumeielewa maana halisi ya Meza ya Bwana. Ikiwa tutakula, basi tayari tutakuwa na nia ya kubatizwa wakati fulani hapo baadae kwani haya yote mawili yanaashiria jambo moja: kujifananisha kwetu na Kristo.

Hakuna kanuni ya ki-imani inayohusika hapa, na ushuhuda ufuatao unadhihirisha hili. Muda mfupi baada ya kuwa tumeokoka, mimi na mke wangu tulifahamu wazi kwamba maisha yetu ni ya Yesu na tulikuwa tayari kumfuata na kumtumikia. Wakati huo, tulikuwa sehemu ya kundi dogo la waumini waliokuwa ndio tu wamemjua Bwana na hatukumfahamu mtu yeyote ambaye angeweza kutubatiza. Kwa kuwa tulikuwa tunajiandaa kutembelea kanisa huko Afrika Kusini, tuliamua kusubiri tukabatizwe huko. Kabla ya kuondoka, tulikuwa tunahudhuria shirika kadhaa ambapo tulishiriki Meza ya Bwana, jambo lililokuwa la muhimu sana kwetu. Je, tungepaswa kusubiri mpaka tubatizwe ndipo tuishiriki Meza ya Bwana? Siamini hivyo

kwani shauku yetu ya kuishiriki ilikuwa sahihi, na utayari wetu wa kutaka kubatizwa ulidhihirisha kujitoa kwetu kwa Bwana, hata kama hatukuwa na uelewa mkubwa wa maana ya ubatizo wakati huo. Kuna mifano mingine mingi ya Wakristo ambao hulazimika kusubiri kwa muda baada ya kuokoka ili wabatizwe kutokana na ratiba za makanisa yao, n.k.

Jambo la muhimu katika kuishiriki Meza ya Bwana ni weupe wa mioyo yetu na shauku yetu ya kujifananisha na mateso na kifo cha Yesu.

## Sura ya IV

# Maombi na Msalaba

### Kuomba sawasawa na mapenzi ya Mungu

Nikitazama huko nyuma, ninakumbuka jinsi katika miaka yangu ya mwanzo nikiwa Mkristo, nilivyotumia muda wangu mwingi wa maombi nikimuomba Bwana kwa ajili ya mahitaji yangu binafsi na ya familia yangu.

Unaweza ukahoji, ‘Kwani kuna tatizo gani hapo?’ Hakuna tatizo, lakini inadhihirisha jinsi nilivyokuwa mchanga kiroho kwani nilitafuta tu mahitaji yangu ya kimwili. Nilikuwa nikitumia maombi ili kujaribu kujitafutia mahitaji yangu binafsi na si vinginevyo.

Unaweza pia ukahoji, ‘Lakini Yesu alisema kwamba tunaweza kuomba lolote kwa Jina lake na Baba atatupatia.’ Basi sasa, kuna ubaya gani kumwomba lolote na chochote tunachokitaka?

Tusisahau kamwe ya kwamba Mungu hayupo tu kutupatia kila kitu tunachokitaka katika sala zetu; bali kinyume chake anataka kutupatia mambo ambayo ni sehemu ya mapenzi yake juu ya maisha yetu. Katika 1 Yohana 5:14, Mtume Yohana anaandika: *“Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia.”*

Kumbuka ya kwamba shauku ya Mungu ni kujenga nyumba ya kiroho. Jambo la muhimu kuliko yote kwake ni kutuona sisi tunabadilika na kumfanana Mwanawe. Unaonaje, basi, tukiliombea Kanisa? Au tukiomba kwa ajili ya ndugu na dada zetu katika Kristo? Au hata kwamba Mungu atuvunje na kutuumba kama apendavyo? Je, hilo halielekei zaidi katika kuomba sawasawa na mapenzi yake?

## Nafasi ya kukua kiroho

Ninakumbuka kisa cha ndugu mmoja katika Kristo aliyekuwa akipitia kipindi kigumu kiuchumi licha ya kuwa alikuwa ameyatoa maisha yake yote kwa Bwana. Alikuwa mtu wa maombi, aliisoma Biblia yake na alikuwa akitoa sana kwa ajili ya kuisaidia kazi ya Bwana. Alinishirikisha moyo wake, kwamba hakuelewa ni kwa nini Bwana alikuwa hajibu maombi yake katika kumpatia mahitaji yake.

Nilimwambia ya kwamba hii haikuwa sababu ya mambo kuwa hivyo, bali inawezekana ulikuwa tu ni wakati wake wa kujaribiwa. Hata hivyo, nilimhakikishia ya kwamba Bwana ni mwaminifu na ya kwamba angempatia mahitaji yake kwa wakati wake. Na hakika, Bwana aliingilia kati kwa wakati wake, lakini pia katika muda huo wa kusubiria yule ndugu alikuwa amekua kiroho.

Sisi sote tunahitajika kupitia nyakati kama hizi tunapotembea na Bwana, iwe ni katika uchumi, ndoa, kazi au mahusiano yetu, kwa sababu tunapoendelea kumngoja Bwana aingilie kati, maamuzi yetu yasiyo sahihi, kukosa imani kwetu na kukosa uvumilivu tuliko nako, yote yanadhihirishwa. Lakini ikiwa tutalinda mioyo yetu na kumruhusu Mungu afanye kazi ndani yetu, hii itakuwa fursa kwetu kukua katika Bwana!

Bwana hutulinda kwa njia ya kipekee na kulingana na Warumi 8:28, tunaweza kuwa na uhakika ya kwamba katika mambo yote yeye hutenda kazi katika kutupatia mema, kwa sababu tunampenda.

Ni lazima tuelewe ya kuwa maombi sio tu njia ya Mungu kututunza kimwili bali pia ni njia ya kuyajenga maisha yetu kiroho.

## Kuuombea Ufalme wa Mungu uendelee

Maombi yetu sikuzote yanapaswa yaambatane na shauku ya kutaka kuuona Ufalme wa Mungu ukiendelezwa kabla ya jambo lingine lolote lile: ujenzi wa kiroho wa Kanisa la Yesu Kristo linapaswa liwe ndilo wazo kuu la kila Mkristo. Katika Matendo 4:29 tunaona jinsi Wakristo katika Kanisa la Kwanza walivyokutana pamoja ili kuomba mapenzi ya Mungu yafanyike.

Hawakushughulishwa na mahitaji yao binafsi, lakini badala yake walimwomba Mungu kwa nguvu wapewe ujasiri wa kuihubiri injili katikati ya mateso yaliyokuwa yakiwakabili. Kwa njia iyo hiyo, Petro alipokuwa gerezani, walimwombea bila kukoma. Hakuna mahali tunapowaona wakiomba kwa ajili ya mahitaji yao binafsi iwe ni kwa ajili ya miili yao au kwa ajili ya kupata vitu. Mahusiano ya jinsi hii na Bwana ni nadra sana siku hizi.

Katika Wakolosai 1:9-11 tunaweza kuona shauku iliyokuwemo ndani ya moyo wa Mtume Paulo kwa ajili ya Kanisa. Maombi yake kwa ajili ya Wakristo yalikuwa ni, *"...ili mjazwe maarifa ya mapenzi yake katika hekima yote na ufahamu wa rohoni…"* makusudi wapate kuenenda *"…kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana."* Je! sisi nasi tunaona haja ya Mungu kuiendeleza kazi aliyoianza ndani yetu kama Paulo alivyoona? Je, tunaona haja ya kuomba kwa ajili ya hili?

Maisha yetu hujengwa kupitia kazi ya Mungu ndani yetu, na hii ndiyo sababu tunapaswa kuikubali hiyo kazi. Maombi si njia ya kukimbia kile Mungu anachotaka kujenga ndani yetu, wala sio njia ya kujipatia wepesi katika maisha yetu ya Ukristo.

Kuna tofauti kubwa kati ya sala ya mtu aliyevunjika na kupondeka na mtu mbinafsi anayetafuta mambo yake mwenyewe. Hii ndiyo tofauti kati ya Mkristo wa rohoni na yule wa mwilini. Mkristo wa rohoni anayeuchukua msalaba wake anajua nini cha kuombea na anaamini kwamba Mungu atashughulikia mahitaji yake pasipo yeye kuyaombea kila wakati. Hata hivyo, Biblia inatuambia ya kwamba Mungu anajua kila hitaji letu hata kabla hatujamwomba (Mathayo 6:8).

Naweza kusema ya kwamba kwa miaka mingi mimi na mke wangu hatujaombea mahitaji yetu binafsi. Ninakumbuka, kana kwamba ilikuwa jana tu, mara baada ya kurejea Mauritius kutoka Afrika Kusini ili kuanza kazi ya

kumtumikia Bwana, kanisa letu lilipangisha kwenye jengo kuukuu kwa ajili ya kuabudia. Lile jengo lilikuwa katika hali mbaya sana na msimu wa masika, mvua ilinyesha ndani kama ilivyonyesha nje! Kwa kuwa tulikuwa tumeuza nyumba yetu kule Afrika Kusini, mimi na mke wangu tungeweza kununua nyingine, lakini tulihisi haukuwa wakati muafaka, kwa kuwa kanisa halikuwa na mahali sahihi pa kuabudia. Kwa hivyo, kwa miaka mingi tuliishi upangajini na kuhama kutoka nyumba moja hadi nyingine, na wakati mwingine tulikuwa zaidi ya familia yetu, kwani mara nyingi tuliweza kuishi na watu wengine wa kanisani mwetu. Hali hiyo iliendelea hadi siku tulipopata mahali pa kujenga jengo la kanisa ndipo tuliponunua nyumba yetu wenyewe. Leo hii tunaishi katika eneo zuri, tulilorithi kutoka kwa babu na bibi zangu. Kama vile mke wangu asemavyo mara nyingi, *"Tungeomba ili tupewe nyumba, tusingefikiria kumwomba Bwana hiki tulicho nacho leo! Tungemwekea mipaka sana..."* Lakini kwa kuwa Mungu aliijua mioyo yetu kwa ajili yake na Ufalme wake, na pia mahitaji yetu, alitupa nyumba kwa wakati wake na kwa njia yake mwenyewe! Hili linaonyesha ya kwamba uamuzi tuliofanya wa kulitanguliza kanisa, badala ya mahitaji yetu binafsi, ulikuwa ndio uamuzi sahihi. Bwana alifanya zaidi ya kile ambacho tungeweza kumwomba au kufikiri, kama Maandiko yasemavyo katika Waefeso 3:20. Mungu wetu ni mwaminifu na anajua jinsi ya kumtunza kila mmoja wetu.

Tunapofika mahali ambapo tuko tayari kuutoa uhai wetu na kuuchukua msalaba wetu, maombi yetu yatabadilika kwa kiwango kikubwa sana. Hayatakuwa tena ya kibinafsi au ya kuombea vitu vya dunia hii, bali tutauombea Ufalme wa Mungu na mambo ya Roho. Haya yatakuwa ni matunda ya kazi ya Mungu ya ndani katika maisha yetu, maisha ambayo sio yetu wenyewe tena bali ni yake. Tutaliombea kanisa, tutaombea kazi ya utume, tutaomba kwa ajili ya mpango wa Mungu na uongozi wake, na mahitaji yetu yatakuwa ya mwisho kwenye hii orodha. Yatakuwa ni kinyume cha 'mimi, mume/mke wangu, watoto wangu, nyumba yangu, gari langu, kazi yangu, fedha zangu, mahitaji yangu binafsi...'

Maombi yetu huonyesha mahali tulipo katika Ukristo wetu. Hebu tulenge kuishi kile ambacho Yesu anatuelekeza katika Mathayo 6:33: *"Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa."*

## Sura ya V

# Toba na Msalaba

Mara tunapozitubia dhambi zetu, na kuweka matumaini yetu kwa Yesu, tunapokea karama ya uzima wa milele. Mfano mzuri wa jambo hili ni pale Mtume Petro alipouhubiria umati mkubwa wa watu siku ya Pentekoste. Alipokuwa akinena habari za Yesu, kuhusu kifo chake msalabani na kufufuka kwake, maelfu ya watu walichomwa mioyo yao na wakauliza wafanyeje. Jibu lake lilikuwa wazi na linatuonyesha njia ya wokovu: *"Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matendo 2:38). Kwa hiyo basi, toba ndiyo mlango wa kuuendea uzima wa milele.

Nakumbuka siku nilipookoka. Nilipogundua ya kuwa mimi ni mwenye dhambi, nilisononeka sana na kuvunjika mbele za Mungu. Nilizitubia dhambi zangu na maisha yangu ya nyuma. Huu uvunjifu ndio ulionisababisha kunyenyekea na kutambua haja yangu ya kumhitaji Yesu.

Lakini je, toba inapaswa kuwa na nafasi gani maishani mwetu tunapokuwa tumefanyika watoto wa Mungu? Tunafanyeje kuhusu dhambi zetu, na udhaifu wetu, tunaposhindwa na kujikuta katika mambo ambayo Mungu hayakubali katika maisha yetu? Sisi sote kuna nyakati tutashindwa na kutenda dhambi, tutakasirika, tutaharibikiwa mioyo na tutakuwa na mawazo mabaya. Je, tutayasahau tu haya na kusonga mbele?

## Toba: ufunguo wa maisha ya Ukristo

Toba inapaswa kuwa sehemu ya maisha yetu ya kila siku, hata baada ya kuwa tumeokoka. Maadam tunaishi katika miili yetu ya kufa, hatutakuwa wakamilifu, na daima tutahitajika kutubu kila wakati tunapotenda dhambi katika kuzungumza, katika kuharibikiwa mioyo, katika utendaji wetu au katika njia nyingine yoyote ile tunapojaribiwa. Lakini je, toba ninayokuwa nayo ninapookoka ni tofauti na toba ninayopaswa kuwa nayo nikiwa Mkristo? Hapana, zote zinatuhakikisha kuhusu dhambi kwa namna ile ile

moja na kutuletea kicho kile kile cha Mungu ambacho ni muhimu katika kuifikia toba ya kweli.

## Kwa nini kumhukumu yeye atendaye dhambi?

Mara nyingi tunapata shida kumkubali ndugu au dada katika Kristo ambaye ameanguka katika dhambi, lakini sivyo ilivyo kwa Mungu kwani yeye anajua kwamba ni sehemu ya maisha yetu. Kama vile Yesu alivyosema katika Mathayo 26:41: *"...roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu."* Mungu anachotaka tu kutoka kwetu ni moyo uliovunjika na kupondeka na uliotubu, kama tunavyoona kwa Daudi. Bwana hakumkataa, ingawa alikuwa amefanya dhambi. Alipotubu kwa dhati, Mungu hakumsamehe tu, bali pia alimrejesha.

Kwa bahati mbaya, Wakristo wengi leo wanajikuta wakisimangwa na kuhukumiwa na wachungaji wao pindi wanapoanguka katika dhambi, kana kwamba wachungaji wenyewe hawawezi kutenda dhambi! Toba inatuhusu sisi ambao ni wachungaji kama ilivyo kwa waumini wote, hakuna asiyehusika. Sisi wachungaji sio wakamilifu na ni hakika kwamba si mara zote tunayatenda mapenzi ya Mungu.

## Mfano wa Wakorintho

Katika waraka wa kwanza wa Paulo kwa Wakorintho tunaona hali legelege Wakorintho waliyokuwa nayo juu ya dhambi ndani ya Kanisa. Wakati waraka huu unaandikwa walikuwa ni watu wa mwilini sana na kulikuwa na mafarakano makubwa miongoni mwao. Ni wazi kwamba hali za mioyo yao ziliwazuia hata wasiweze kumkemea ndugu aliyekuwa katika hali ya kutisha ya dhambi, kama inavyoelezewa katika sura ya tano. Katika waraka wake wa kwanza Paulo anaelezea masikitiko yake juu ya wao kutokuhuzunikia ile hali. Anawaambia ya kuwa alitarajia kinyume chake kutoka kwao: ya kwamba wangefadhaika kutokana na hali ya aibu iliyokuwemo ndani ya kanisa.

Kutokana na hali hiyo, uhusiano baina ya Paulo na Wakorintho ulikuwa umedorora na hili lilimsononesha sana. Hakuwa amepata majibu ya aina yoyote kutoka kwao kwa waraka wake wa kwanza, lakini alikuwa akitarajia jambo moja tu: ya kwamba uhusiano wao na yeye ungerejeshwa, ya kwamba wangeirudia injili na tatizo lile lingepatiwa ufumbuzi.

Katika waraka wake wa pili, hasiti kuwashirikisha huzuni yake ya awali, kwani kanisa la Korintho lilianzishwa kutokana na huduma yake: *"Tupeni nafasi mioyoni mwenu. Hatukumdhulumu mtu ye yote, wala kumharibu mtu, wala kumkaramkia mtu."* (2 Wakorintho 7:2). Kwa maneno mengine, Paulo anawauliza, 'Ni kwa nini kuwepo na matengano ya aina yoyote kati yetu?' Anawafafanulia ya kuwa ile hali ya dhambi na maamuzi yao ndiyo mambo yaliyowatenganisha rohoni. Inawezekana waraka wake wa kwanza ulionekana kuwa ni mkali, lakini hakuwa na budi kuwaambia ukweli, hata kama ukweli huo ungesababisha kanisa kugawanyika iwapo wangekataa kutubu. Lakini, kama vile Tito alivyotoa taarifa baada ya kurejea kutoka Korintho, walitubu na kuikiri hali yao, na Paulo anafurahia anaposema: *"...akituarifu habari ya shauku yenu, na maombolezo yenu, na bidii yenu kwa ajili yangu, hata nikazidi kufurahi."* (2 Wakorintho 7:7).

Matokeo yake ni kwamba Wakorintho walipata shauku na bidii mpya ya kushirikiana na Paulo. Kwa kuwa sasa walikuwa wamoja naye, tena rohoni na moyoni, aliweza kulishughulikia lile jambo kwa njia ambayo iliweza kumvuta ndugu aliyetenda dhambi kuweza kutubu. Inafaa kuuliza, je, ni kwa jinsi gani hili badiliko la moyo na hali ya kutubu vilivyojitokeza? Jibu ni rahisi: Ni kwa kuhakikishwa na Roho pekee!

Kuhakikishwa dhambi na toba tunakoshuhudia kwa Wakorintho kutokana na hili jambo ilikuwa sawa na jinsi walivyotubu wakati wanaokoka na hali hii inapaswa iwe endelevu leo kwa kila Mkristo aliyezaliwa upya na Roho wa Mungu.

Katika kuhitimisha, Paulo anawaambia Wakorintho: *"Kwa sababu, ijapokuwa naliwahuzunisha kwa waraka ule, sijuti; hata ikiwa nalijuta, naona ya kwamba waraka ule uliwahuzunisha, ingawa ni kwa kitambo tu. Sasa nafurahi, si kwa sababu ya ninyi kuhuzunishwa, bali kwa sababu mlihuzunishwa, hata mkatubu. Maana mlihuzunishwa kwa jinsi ya Mungu, ili msipate hasara kwa tendo letu katika neno lo lote."* (2 Wakorintho 7:8-9). Anafafanua katika mstari unaofuata kwa kusema, *"Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba iletalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti."*

## Toba ya kweli: matunda ya kujutia

Toba ya kweli siyo kanuni au mbinu. Ni uhalisia ambao kila Mkristo anapaswa kuuishi. Sio suala tu la kutamka maneno yanayoendana na Maandiko bali

ni jambo linalohitaji badiliko la kweli la nia na uvunjifu wa kweli wa ndani, unaompelekea Mkristo kujinyenyekeza mwenyewe. Lakini, kwa bahati mbaya, Wakristo wengi na hata wachungaji hawajatubu kwa jinsi hii kwa muda mrefu sana.

Katika Zaburi ya 51, Daudi anaelezea wakati wa toba ya kweli aliokuwa nao mbele za Bwana. Tunaweza tukahisi kuvunjika kwake na huzuni yake iliyokuwa kwa njia ya Mungu. Anaandika, *"Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika; moyo uliovunjika na kupondeka, Ee Mungu, hutaudharau."* Anakiri dhambi yake mbele za Bwana na kumuomba msamaha, akisema, *"Maana nimejua mimi makosa yangu..."* na tena, *"Ee Mungu, uniumbie moyo safi..."* Hii ndiyo aina ya toba Mungu anayotaka Kanisani.

## Toba huleta urejesho

Panapotokea jambo kati yangu na mke wangu au ndugu au dada katika Kristo, mara nyingi huwa nahisi kama ukuta umejengeka kati yetu. Toba huushusha huo ukuta na hurejesha amani na furaha. Kwanza huja hali ya huzuni tunapotambua ya kwamba tumemhuzunisha Mungu au kumkosea mtu, na wakati huo huo tunahisi hali ya kuvunjika inayotuwezesha kusawazisha mambo. Tunasukumwa kusema, 'Sikupaswa kusema au kufanya vile' na huzuni yetu kwa kuwa tumemsononesha Mungu na kumuumiza mtu huleta kuvunjika kunakotusababisha kutubu.

Ni wanaume wangapi wa Kikristo wasioweza kutubu kwa wake zao? Bila shaka nyakati za kufanya hivyo ni nyingi, iwe ni kutokana na kuharibika mioyo, hasira, kutokujali, ugumu wa moyo, n.k. Na bila shaka, vivyo hivyo wake nao wanapaswa kutubu kwa waume zao pia! Kukosa toba ni tatizo kubwa Kanisani leo.

Ni wazi kwamba kiburi chetu hupata pigo tunapokiri kushindwa kwetu na mapungufu yetu. Ni vigumu... Lakini kuna uhuru mkubwa sana unaopatikana tunapokubali! Kutofautiana kati ya mume na mke mara nyingi huzaa mabishano kila mtu anapong'ang'ania msimamo wake. Hata hivyo, ni jambo la kipekee tunapokubali kushindwa na hasa ikiwa tulifikiri tuko sahihi!

Sitasahau siku ambayo mimi na mke wangu tulipogombana. Hatukusuluhisha lolote na niliamua kuondoka na kwenda kazini badala ya kujaribu kulishughulikia lile tatizo. Ilikuwa ni mwanzoni kabisa nilipokuwa nimeanza

kufahamu umuhimu wa kuuchukua msalaba wangu, kujinyenyekeza na kumruhusu Bwana kunivunja na kunibadilisha. Nilipokuwa ninaondoka na gari langu, nilihisi ya kuwa amani yangu ilikuwa imeniacha. Roho Mtakatifu alinikabili kwa nguvu na nikatambua ya kuwa nilikuwa nimemwumiza mke wangu na nilipaswa kurudi na kutubu mbele zake. Lakini kujinyenyekeza mbele zake ilionekana kama mlima kwangu! Kwa wakati ule, nilikuwa nimetumika kama mchungaji kwa miaka kadhaa, lakini niligundua ya kwamba sikuwahi kumwomba mke wangu msamaha hata siku moja; na Bwana tu ndiye aliyejua ni mara ngapi ningepaswa kuwa nimefanya hivyo! Niligeuza gari na nikarudi nyumbani. Nilijinyenyekeza mbele zake kwa moyo wa dhati na kumwomba anisamehe. Mke wangu hakuamini! Bila shaka, huu ulikuwa ni mwanzo wa mabadiliko katika ndoa yetu.

Muda si mrefu baada ya hapo, Bwana alianza kuurejesha uhusiano wetu. Mke wangu anapolizungumzia hilo tukio, mara zote huwa anasema, *"Ilikuwa ndiyo mara yangu ya kwanza kuuhisi moyo wa Miki ya kwamba alikuwa haombi msamaha kwa kuwa tu imeandikwa."*

Toba ni jukwaa lisilokuwa la kawaida ambalo Mungu hutumia kufanya kazi maishani yetu. Hurekebisha, hurejesha, na hutengeneza palipoharibika.

## Toba huleta uhai

Ni nini kitakachorejesha toba ya kweli Kanisani leo? Ni ujumbe wa msalaba, unaonena juu ya kuyafananisha maisha yetu na Yesu.

Ni rahisi sana kwa Kanisa kuasili roho ya kidini na kuhisi kwamba halina haja tena ya kutubu mbele za Bwana. Hata hivyo ujumbe wa msalaba sikuzote utatuelekeza kutubu na kulinda moyo safi. Ujumbe wa mara moja moja kuhusu toba hakika hauwezi kulifanikisha hilo. Hii ndiyo maana roho wa kweli wa injili, ambao ni ujumbe wa msalaba, ule wa Yesu Kristo aliyesulubiwa, ni sharti udumishwe Kanisani!

Tukirejea mfano wa kanisa lililokuwa Korintho, toba ilileta nini katika maisha yao? Ilileta uhai. Haya ndiyo matunda ya moja kwa moja ya ujumbe wa msalaba, yaani, kujifananisha kwetu na Kristo katika mauti yake hutuwezesha kuubeba uhai wake.

Toba hii ilileta nia mpya, msimamo mpya, uhuisho na upatanisho katika roho. Ilileta pia hali ya kuichukia dhambi, kicho cha Mungu, shauku ya dhati na bidii mpya ya kumwandamia Bwana, pamoja na shukrani nyingi kwa kile Mungu alichokuwa amekifanya mioyoni mwao kupitia jambo lile, ingawa lilikuwa gumu. Kwa mara nyingine tena mambo yakawa wazi rohoni kati ya Paulo na Wakorintho. Kila kitu kikarejea mahali pake na wakapata uhai na amani ya Yesu tena.

Toba inapaswa kuwa kitu cha kawaida katika maisha yetu ya kila siku. Ndiyo njia pekee itakayorejesha uhusiano wetu na Mungu na watu pia. Hatupaswi kamwe kuona aibu kutubu. Kutubu kamwe sio kushindwa, wala sio ishara ya udhaifu. Kinyume chake, ni ushindi. Ni njia tuliyopewa tuweze kujinyenyekeza na kumruhusu Bwana kutuinua. Ni jambo lisiloepukika katika maisha ya Ukristo si tu katika kuilinda amani bali pia kwa ajili ya ukuaji wetu rohoni. Dhambi hutuondolea furaha ya wokovu bali toba huirejesha hii furaha na kutuwezesha kukua katika kuulekea utu uzima rohoni.

## Sura ya VI

# Msamaha na Msalaba

*"Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu."* (Mathayo 6:14-15).

Ingawa tunafahamu ya kwamba Bwana hutusamehe, mara nyingi sisi tunapata shida kuwasamehe wengine. Tunasamehe baadhi ya mambo, lakini tunashindwa kusamehe mengine, jambo ambalo ni tatizo kubwa kwani Yesu mwenyewe anatuonya ya kwamba Baba hatawasamehe wale wasiosamehe.

## Mifano kutoka kwa Yesu na mitume

Tunapouzungumzia ujumbe wa msalaba, tunazungumza juu ya msamaha. Yesu ndiye kielelezo kamili cha hili: alikubali kila kitu na kusamehe maovu yote aliyotendewa.

Yesu kila wakati aliwasamehe maadui zake bila kuufanya moyo wake kuwa mgumu ingawa alishtakiwa kwa uongo, akapigwa na hatimaye kuuawa. Aliuendea msalaba akiwa na moyo mweupe, *"wala hakufunua kinywa chake..."* (Isaya 53:7). Kwa njia hii akaukamilisha ushindi wake.

Alipokuwa akiteswa msalabani, na kuaibishwa kwa matusi, bado aliomba, *"Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo."* (Luka 23:34). Alikiishi kile alichohubiri hadi mwisho.

Stefano alikuwa na moyo huo huo alipopigwa mawe kwa ajili ya kuihubiri injili. Akiwa na moyo uliojaa neema, alionyesha msamaha ule ule aliouonyesha Yesu kwa watesi wake kwa kuomba, *"Bwana, usiwahesabie dhambi hii."* (Matendo 7:60). Stefano alikuwa mtu wa rohoni. Alielewa maana ya kuuchukua msalaba na kumfuata Yesu. Alichagua kuihubiri injili na kujifananisha na Bwana kuliko kujitetea na kubaki na uchungu na kutobeba msamaha kwa watesi wake. Kwa roho iliyovunjika alimuomba Mungu kwa ajili yao.

Mtume Paulo naye pia alikabiliana na upinzani mkubwa katika huduma yake, huku wahubiri wakisimama kumpinga pamoja na injili yake. Hata Wakorintho walivutwa na mashtaka ya uongo yaliyoelekezwa kwake na watu wengine. Licha ya hayo yote, yeye hakuwa na uchungu nao wala na hao wahubiri waongo. Si hilo tu, bali alifurahi pia kama tunavyoona katika Wafilipi 1:18 anaposema: *"Yadhuru nini? Lakini kwa njia zote, ikiwa ni kwa hila, au ikiwa ni kwa kweli, Kristo anahubiriwa; na kwa hiyo nafurahi, naam, nami nitafurahi."*

Je, tunapaswa tuuige kiasi gani mfano wa jinsi hii katika kuubeba msalaba!

## Msamaha chini ya Agano Jipya

Katika Hotuba ya Mlimani, Yesu aliufundisha umati juu ya uwezekano wa kuishi aina tofauti ya maisha. Aliilinganisha hii njia mpya na njia ya zamani chini ya Agano la Kale. *"Mmesikia kwamba imenenwa, Jicho kwa jicho, na*

*jino kwa jino; Lakini mimi nawaambia, Msishindane na mtu mwovu; lakini mtu akupigaye shavu la kuume, mgeuzie na la pili. Na mtu atakaye kukushitaki na kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia."* (Mathayo 5:38-40).

*"Mmesikia kwamba imenenwa, Umpende jirani yako, na, Umchukie adui yako; lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi, ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki. Maana mkiwapenda wanaowapenda ninyi mwapata thawabu gani? Hata watoza ushuru, je! Nao hawafanyi yayo hayo? Tena mkiwaamkia ndugu zenu tu, mnatenda tendo gani la ziada? Hata watu wa mataifa, je! Nao hawafanyi kama hayo? Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu."* (Mathayo 5:43-48).

Kuwasamehe maadui wa mtu, jambo ambalo lisingewezekana chini ya Agano la Kale, sasa linawezekana chini ya Agano Jipya. Yesu mwenyewe alifanyika kielelezo chetu katika hili pale alipokufa msalabani.

## Msamaha: tendo la kila siku

Msamaha ni jambo tunalopaswa kuliishi kila siku na kuna gharama ya kulipa katika kunyenyekea na kuvunjika. Tunapaswa tufike mahali ambapo tutajishughulisha tu na mambo ya wakati wa sasa na si ya nyuma. Kwa maneno mengine, nikiishasamehe mambo ya nyuma ninaweza kusonga mbele na kuwa na uwezo wa kusamehe kila siku. Kila Mkristo anapaswa aishi kwa jinsi hiyo: akiwa huru na hali ya kuangalia mambo ya nyuma, iwe ni ya wiki moja, au hata siku moja, kwa sababu suala la kusamehe limekuwa zoezi la kila siku kwake. Kila siku ninasamehe, na kila siku inanigharimu!

Mara nyingi sana hatuelewi ya kwamba tunapaswa kuwa tayari kuwasamehe wake zetu, watoto wetu, wazazi wetu, wafanyakazi wenzetu, mwajiri wetu na hata wale wanaotukataa na kututesa... Ni lazima tusamehe wote wanaotuudhi, wanaotudharau na kutuumiza, hata wale wanaotusingizia mambo ambayo hatujafanya, wale wanaotudhihaki na wakorofi. Nina hakika utakubaliana nami ya kwamba sisi sote tunakabiliana na mambo ya jinsi hii kwa nyakati fulani maishani mwetu. Mume wako atakuinukia bila sababu, mke wako atakusukumizia mbali... haya ni mambo ya kila siku! Kwa bahati mbaya, tunajikuta jua linakuchwa tukiwa bado na uchungu mioyoni mwetu na mizigo mizito mabegani mwetu.

Ili kuilinda mioyo yetu, ni muhimu tuenende katika hali ya kusamehe muda wote. Inasikitisha ya kwamba tunaweza kuamini ya kwamba mioyo yetu i wazi mbele za Bwana wakati tumebeba kutokusamehe. Hebu tujikumbushe mara nyingine tena ya kwamba Yesu alituonya ya kwamba ikiwa hatutawasamehe watu, Baba yetu wa mbinguni naye hatatusamehe. Hatuwezi kuendelea kuishi hivyo. Ni lazima tusalimishe haki yetu ya kujitetea na kujihesabia haki, na tusamehe.

## Madhara ya kutokusamehe

Kutokusamehe ni sawa na mtu kutembea akiwa amefungiwa chuma nzito kwenye mnyororo, na hili litamzuia katika utumishi wake kwa Mungu. Tunaposhindwa kusamehe, iwe ni katika jambo kubwa au dogo, tunaifanya mioyo yetu kuwa migumu. Lakini bado, Mungu anataka tuwe na moyo mwororo, moyo ambao anaweza kuufanyia kazi na kuubadilisha. Mungu hawezi kufanya lolote na moyo mgumu. Na tunapoendelea kushikilia kosa, tunakuwa katika hatari ya kuanguka kiroho.

Kutokusamehe ni kitu kiovu kinachotutafuna, na kutunyang'anya baraka za Bwana. Tukitazama kwa karibu, tunaona ya kwamba mtu aliyetukosea na akatubu, au ambaye wakati mwingine hana hata taarifa ya kwamba ametukosea, anakuwa na amani kuliko mtu aliyekosewa na ambaye hawezi kujinyenyekeza na kusamehe. Yeye asiyesamehe hubaki akiwa mtumwa wa yule aliyemkosea kwa kushikilia kosa lake, na anatembea katika kushindwa. Ni sawa na kujiruhusu tuongozwe na kiburi chetu na mwili ule ule ambao Bwana anatamani kuuvunja.

Wakristo wengi wameelemewa kwani wanatembea wakiwa 'wamewabeba' watu wote ambao wameshindwa kuwasamehe. 'Alisema hiki, alifanya kile, siwezi kumsamehe...' Hatukuitwa 'kuwabeba' watu kwa jinsi hii maishani mwetu! Lakini tunayakumbuka yote waliyosema na waliyotutendea! Mara nyingine tunaenda mbali zaidi na hata kuyashiriki manung'uniko yetu na watu wengine na kunena vibaya juu ya matatizo yetu na watu, bila kuelewa ya kwamba tunapanda 'mbegu mbaya' mioyoni mwao. Tunaposhindwa kusamehe, mara zote tunajaribu kujihesabia haki kwa kuwakosoa wale waliotuumiza au kutuudhi. Badala ya kujenga, tunaishia kubomoa. Je, hivi ndivyo tunavyotaka kuyaishi maisha yetu?

Kila siku kila Mkristo ana uamuzi wa kusamehe au kuufanya moyo wake kuwa mgumu. Mara nyingi, Mkristo anaposema jambo linalomuumiza mwenzake, yule wa pili ataufanya moyo wake kuwa mgumu na atamsubiri yule aliyemkosea aje kutubu ili aweze kumsamehe. Lakini msamaha wa kweli hautegemei matendo ya yule mwingine. Tumeitwa kuachilia maumivu yetu na kuwasamehe wanaotuudhi, wawe wameyatubia matendo yao au la, ili kuiweka mioyo yetu ikiwa safi na yenye amani. Hili si jambo rahisi, lakini ni uamuzi tunaopaswa kuufanya ili kuhakikisha hakuna jambo linalouzuia ushirika wetu na Mungu au kutukosesha baraka alizotuwekea.

## Kumsamehe kila mtu

Yesu alisemaje pale msalabani? *"Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo."* Mara nyingi tunasahau ya kwamba adui anaweza kutumia wasioamini kuyatimiza malengo yake. Lakini sisi, badala ya kuzing'amua mbinu za adui, tunabaki kumuangalia yule mtu aliyetukosea. Tunaangalia namna walivyotuudhi, tunaangalia hali za mioyo yao kwetu. Lakini je, tunataraji nini kutoka kwa mtu asiyemjua Bwana? Mara nyingi watatumika tu kama vyombo vya adui! Watu wanaposimama kinyume nasi na kutushuhudia kwa uongo, je, tunapaswa tuwatendeje? Tunapaswa kuwasamehe! Ndio wito wetu. Ninawahakikishieni ndugu na dada zangu katika Kristo, hatuna uchaguzi katika hili suala: msamaha hauna mbadala. Sio sheria bali ni kuuitikia wito wa Roho Mtakatifu utakaomruhusu Mungu kuendelea kutuvunja na kutuumba upya.

## Msamaha huleta uhuru

*"Mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo na ninyi."* (Wakolosai 3:13). Mungu ni mwenye neema kwetu. Yeye hututia nguvu ili tuweze kutembea pamoja naye, kuuchukua msalaba wetu na kusamehe. Ni lazima tumruhusu akivunje kiburi chetu ili tuishi kwa uhuru, pasipo kushikilia neno dhidi ya mtu awaye yote. Je, ni kipawa cha aina gani na ni neema iliyoje kufanyika watoto wa Mungu! Tunaweza kusamehe kila siku. Leo, kesho, baada ya wiki, kila wakati tutahitajika kusamehe na kuachilia.

Tunapaswa tujifunze kusamehe haraka, na tusiruhusu uchungu wowote au kinyongo kuota mizizi mioyoni mwetu, makusudi tuwe huru na watu wote.

Kinachohitajika tu ni utayari wetu wa kujinyenyekeza! Na hii ndiyo sehemu ya msalaba ambayo Yesu anatuhitaji tuichukue kila siku.

## Kusamehe bila mipaka

Alipokuwa akijibu swali la Petro, Yesu alisema tunapaswa kusamehe hata saba mara sabini. Kwa maana nyingine, tunapaswa tusamehe hata kama ni kosa lililojirudia. (Mathayo 18:21-22). Kwa kawaida, huwa tunaishia kuwa na moyo mgumu dhidi ya mtu anayetukosea tena na tena. Ni nani anayependa kuumizwa au kuaibishwa? Lakini hili ndilo jambo Mungu analotaka tulikubali. Na tunaposhindwa kusamehe papo kwa papo, Roho Mtakatifu huweza kutunong'oneza ya kwamba kufanya hivyo ndilo jambo sahihi ikiwa kweli tunataka kumpendeza Mungu.

Siku za nyuma kidogo, mama mmoja kanisani mwetu alipita mbele ili aombewe. Mke wangu alipokuja kumwombea aligundua kwa haraka ya kuwa yule mama alikuwa amebeba kutokusamehe moyoni mwake. Alipoulizwa, alikiri ya kwamba alikuwa amebeba fundo moyoni dhidi ya mume wake tangu mwanzo wa ndoa yao ambapo ni zaidi ya miaka arobaini iliyopita! Alishindwa kumsamehe. Mke wangu akamweleza ya kwamba, ikiwa hakuwa tayari kumsamehe mume wake, hapakuwepo na sababu ya kumwombea. Yule mama akasema hakuwa tayari kufanya hivyo, na mke wangu akaendelea kuwaombea watu wengine waliokuwa wamejitokeza. Baada ya muda, yule mama akamwita mke wangu na kusema alikuwa tayari kuchukua hatua ya kumsamehe mume wake. Miezi michache baadaye, mume wake akafariki. Ni neema iliyoje kwamba aliweza kumsamehe mume wake kwa wakati! Ni ushindi ulioje... Zaidi ya hapo, kabla hajafariki mume wake alikuwa amehisi badiliko kwa mke wake, na wakawa wameshuhudia uhusiano wao ukirejeshwa upya.

Inashangaza kuona jinsi ambavyo Wakristo wanavyoweza kubaki wamefungwa na wale waliowaumiza au kuwaudhi, mara nyingine wakibeba lawama kwa miaka mingi, bila kuona jinsi kutokusamehe na ugumu wao wa moyo unavyowazuia wasiweze kutembea na Bwana.

Tunapoyaangalia maisha yetu wenyewe, tunaona ya kuwa Baba yetu wa mbinguni mara nyingi ni mvumilivu sana, kwani hutusamehe makosa yetu yale yale, hali zile zile za mioyo yetu mibaya, hasira zile zile, ukosoaji wa watu

ule ule, kuwahukumu watu kule kule, tena na tena... Tunawezaje kuufurahia msamaha wake na wakati huo tukikataa kumsamehe mtu aliyetuudhi?

## Msamaha: chanzo cha uponyaji

Msamaha ni sehemu ya maisha yetu ya Ukristo inayoweza kutatua mambo mengi na hasa katika maisha ya mtu binafsi. Kusamehe huponya na kuturejesha upya, lakini pia ni nafasi ya Bwana kutuvunja na kutuumba upya katika sura ya Kristo.

Katika kila jaribu linalojitokeza, ninapaswa kujiuliza: ni jambo gani Bwana analojaribu kufanya moyoni mwangu kwa wakati huu? Je, nijiangalie hali yangu au nimwangalie yule anayenikosea? Ikiwa tuko tayari kuuchukua msalaba wetu, kila mara Roho Mtakatifu atatusaidia kujinyenyekeza, kusamehe na kuachilia. Ikiwa tunataka kuenenda katika moyo safi na kumpendeza Bwana, maisha yetu yatajaribiwa kwa jinsi hii mara kwa mara. Msalaba ndio njia pekee ya kuupata ushindi na kubaki na amani na furaha moyoni. Hakuna mbadala. Huu ndio msingi wa maisha ya Mkristo.

### Sura ya VII

# Neema na Msalaba

Mungu ameudhihirsha wema wake kwa watu wote kupitia wokovu aliotupatia katika Yesu Kristo. Hata hivyo, kuna eneo lingine la neema yake, iliyopo kwa ajili yetu baada ya kuwa tumeokoka. Ni nguvu ya Uungu, na chanzo cha kimuujiza chenye nguvu tunayoweza kuchota wakati wowote katika maisha yetu ya Ukristo; itakayotuwezesha kukabiliana na mitihani na majaribu ambayo hayana budi kuja kwetu. Maisha ya Mtume Paulo yamejaa mifano ya jinsi hiyo.

## Neema kwa ajili ya wokovu

Neema kwanza kabisa ni kipawa tusichostahili kitokacho kwa Mungu: *"…ingawa hapo kwanza nalikuwa mtukanaji, mwenye kuudhi watu, mwenye*

*jeuri, lakini nalipata rehema kwa kuwa nalitenda hivyo kwa ujinga, na kwa kutokuwa na imani. Na neema ya Bwana wetu ilizidi sana, pamoja na imani na pendo lililo katika Kristo Yesu."* (1 Timotheo 1:13-14). Paulo anakiri jinsi alivyopokea neema ya Mungu kwa wingi siku alipookoka. Alijiona kuwa ni kielelezo cha hiyo neema hasa kwa kuwa alikuwa mtu mwovu kupindukia kabla ya wokovu wake. Hebu fikiria jinsi alivyowatesa Wakristo wa Kanisa la Kwanza, hata akisimamia na kushuhudia Stefano akipigwa mawe, kama yeye mwenyewe anavyoelezea katika Matendo 22:4, *"nikawaudhi watu wa Njia hii hata kuwaua, nikawafunga, nikiwatia gerezani, wanaume na wanawake..."* Lakini, Bwana bado alichagua kujidhihirisha kwake, hata kumfanya kuwa mtume kwa Mataifa na kumtumia kuandika nusu ya Agano Jipya!

Mungu anaweza kumuokoa mtu yeyote kwa sababu Yesu alikufa msalabani kwa ajili ya wanadamu wote. Wokovu basi unapatikana kwa kila mtu kutokana na neema ya Mungu pekee.

## Neema ya Kumtumikia Yesu katikati ya Mateso

*"Na makusudi nisipate kujivuna kupita kiasi, kwa wingi wa mafunuo hayo nalipewa mwiba katika mwili, mjumbe wa Shetani ili anipige, nisije nikajivuna kupita kiasi. Kwa ajili ya kitu hicho nalimsihi Bwana mara tatu kwamba kinitoke. Naye akaniambia, Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu."* (2 Wakorintho 12:7-9).

Hapa tunasoma jinsi Mtume Paulo alivyomsihi Bwana amwondelee 'mwiba katika mwili'. Ni wazi kwamba ilikuwa ni vigumu mno kwake kukabiliana na hali hiyo, lakini jawabu la Bwana, *"Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu"*, lilimtia nguvu na kumfariji. Akaelewa ya kwamba imani yake ilikuwa ikijaribiwa na ilikuwa ni sehemu ya msalaba aliopaswa kuubeba. Akaelewa pia ya kuwa hali hiyo isingeweza kumzuia kwa namna yoyote kumtumikia Mungu, huku akijua kwamba neema ya Mungu ilikuwepo kumsaidia kuendelea kumtumikia Bwana. Zaidi ya hayo, huu mwiba ulikuwa ni njia ya kumfanya ajifananishe na Kristo katika mateso na kifo chake, na akaelewa ya kwamba Bwana alikusudia kuutumia kumbadilisha azidi kufanana naye. Huu ni ufunuo wa ajabu kwa Kanisa la leo, hasa wakati wengi wanapoonekana kutofahamu ya kuwa neema ya Mungu ipo kwa ajili yetu pale tunapokuwa tayari kuuchukua msalaba wetu na kumfuata Yesu.

Paulo anahitimisha kwa kusema ya kuwa nguvu ya Mungu ingedhihirishwa ndani mwake kupitia udhaifu wake na majaribu ambayo yangempata. Anaenda mbali zaidi hata kusema anafurahia nyakati ngumu kwa sababu anaitamani nguvu ya Kristo kuliko kitu chochote katika utumishi wake, na yuko tayari kuuchukua msalaba wake kwa ajili ya hilo. Mtu yeyote anayeelewa wito wa Mungu, awe ni mshirika, mchungaji, au aliyeko kwenye jukumu la aina yoyote katika huduma, anaweza tu kumtumikia Mungu kupitia nguvu zake na uhai wa Kristo. Ni lazima tuelewe ya kwamba gharama tunayodaiwa ni kuuchukua msalaba wetu, na iwapo tutakubali kufanya hivyo basi neema ya Mungu itatutosha.

Ufunuo wa neema hii na uhakika wa kuwa tunaweza kuzitumainia nguvu za Mungu wakati wowote hutuwezesha kuzikubali nyakati ngumu, kuuchukua msalaba wetu na kumruhusu Bwana kutuvunja na kutufinyanga kupitia nyakati hizi. Haiwezekani kufanya hivyo kwa nguvu zetu wenyewe, bali neema ya Mungu hutusaidia kukabiliana na hali za aina yoyote. Hutuwezesha wakati huo anapokuwa akifanya kazi ya kina ndani ya mioyo yetu.

## Neema katika kujaribiwa

*"Kwa maana mmepewa kwa ajili ya Kristo, si tu kumwamini, bali pia kuteswa kwa ajili yake..."* (Wafilipi 1:29).

Andiko hili linanikumbusha dada mmoja ambaye alikuwa mshirika katika kanisa letu ambaye mume wake alikuwa sio Mkristo. Mume wake aliyafanya maisha ya dada huyu kuwa magumu sana na alimtesa sana kwa sababu ya imani yake na kujitoa kwake kwa Bwana. Nilikuwa nikishangazwa na namna dada yule alivyoweza kuchukuliana na hali hiyo, na mara nyingi niliwaza kwamba mimi mwenyewe nisingeweza kuvumilia mambo aliyokuwa akifanyiwa. Hata hivyo, kwa kadiri Mungu alivyoleta ufunuo wa nguvu ya neema yake ndani ya moyo wangu, nilielewa kuwa katika kuteswa kwake kwa ajili ya Kristo, Mungu aliweza kumpatia yule mama nguvu na neema aliyohitaji. Na katika kipindi hicho chote, nilimshuhudia akikua kiroho.

Kuna idadi kubwa ya Wakristo waliopitia katika nyakati za dhiki kubwa kwa ajili ya imani yao, na ambao walikiri jinsi walivyoishuhudia neema ya Mungu katikati ya majaribu hayo. Msalaba ambao Yesu anatutaka tuubebe daima huambatana na neema ya Mungu na kazi yake mioyoni mwetu.

Mtume Paulo anakiri kwamba neema ya Mungu ilimsaidia kupitia mitihani na majaribu yote aliyokabiliana nayo, mojawapo zikiwa nyakati alizotumika jela. *“Lakini kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo; na neema yake iliyo kwangu ilikuwa si bure, bali nalizidi sana kufanya kazi kupita wao wote; wala si mimi, bali ni neema ya Mungu pamoja nami.”* (1 Wakorintho 15:10). Alikuwa tayari kuzifia tamaa zake mwenyewe na kuusulubisha mwili wake kwa sababu alifahamu ya kuwa neema ya Mungu ilikuwepo daima, muda wote, kumwezesha kusimama imara hadi mwisho. Katika 2 Timotheo 4:7, anasema: *“Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda.”* Kwa maana hiyo basi, maisha yetu ya Ukristo hayana utofauti na yale ya Paulo; ni vita visivyokoma, ambapo imani yetu sikuzote inajaribiwa, ili tuweze kukua kiroho.

Ni nadra sana kusikia maneno ‘neema kwa ajili ya kuteseka’ yakitamkwa katika mikusanyiko ya Kikristo siku hizi, na sababu ya hili ni kwa kuwa Wakristo hawatambui tena nafasi msalaba unayopaswa kuchukua maishani mwao. Ikiwa tumedhamiria kusonga mbele, neema ya Mungu siku zote itakuwepo kutusaidia kukabiliana na kila mtihani, jaribu, shida au mateso bila majuto yoyote, huku tukijua kwamba, *“...katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema...”* (Warumi 8:28).

Kama kuna jambo moja tunalohitaji katika kutusaidia kuuchukua msalaba wetu kila siku, hakika ni ufunuo wa nguvu ya neema ya Mungu maishani mwetu!

## Sura ya VIII

# Majaribu na Msalaba

*"Kwa kuwa hatuna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi."* (Waebrania 4:15). Ni dhahiri kutokana na kifungu hiki kwamba Yesu alijaribiwa kama sisi nasi tunavyojaribiwa. Katika Sura ya 4 ya injili ya Luka, tunaona jinsi ambavyo Shetani alimjaribu Yesu mara tatu jangwani ili amtii yeye badala ya kuufuata mpango wa Baba yake. Licha ya mipango ya Shetani, Yesu kamwe hakuanguka katika majaribu, bali daima alitembea katika utakatifu na ukamilifu.

Unaweza kuuliza, 'Je, ni jambo la kawaida kuhisi kujaribiwa?' Jibu ni ndiyo! Kulingana na 1 Wakorintho 10:13, hakuna jambo la ajabu juu ya kujaribiwa, na mara zote kuna njia ya kutokea. Kama mithali mojawapo ya Kichina isemavyo, 'Huwezi kuzuia ndege wa huzuni wasipite juu ya kichwa chako, lakini hakika waweza kuwazuia wasijenge viota kwenye nywele zako.' Kwa hivyo, jaribu sio dhambi, tusiposhindwa nalo.

## Miili yetu na majaribu

Popote tunapoenda siku hizi, tunajaribiwa kwa njia nyingi, iwe ni mitaani, madukani, au hata tunaposoma gazeti, kuangalia televisheni, n.k. Na majaribu yanaongezeka kila kukicha. Roho inayotawala duniani inafanya kazi kuhakikisha mwanadamu anakaa gizani, lakini pia iko kazini kuwavuta Wakristo katika dhambi.

Tunajaribiwa na kile tunachokiona, tunachokisikia, kuwaza na hata kubuni katika fikra zetu, na ndio maana tuna kila sababu ya kuepuka maeneo ambapo majaribu yana nguvu, na ambapo Shetani anatumia kila hila kuivuta miili yetu, kama Mtume Paulo anavyosema katika Wagalatia 5:17: *"Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana..."*

*“Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti.”* (Yakobo 1:14-15). Hapa, Mtume Yakobo anaelezea waziwazi mlolongo wa mambo yanayoanzishwa tunapokubaliana na tamaa zetu za kimwili. Ni jukumu la kila mmoja wetu kuzipinga tamaa zinazopelekea kutenda dhambi.

Unaweza ukasema, ‘Hilo ni rahisi kusema kuliko kutenda.’ Ni kweli! Najua jinsi nilivyo dhaifu, jinsi nilivyo mtu wa mwilini, na jinsi nilivyo hatarini kutenda dhambi, kama Paulo anavyoeleza katika Warumi 7:14. Lakini bado jawabu linabakia kuwa ni katika kuuchukua msalaba wetu, kuwa tayari kuisulubisha miili yetu pamoja na tamaa zake na shauku zake, huku tukiwa tayari kufanya lolote linalohitajika ili kuwa huru mbali na dhambi. Hiyo ndiyo maana halisi ya kuifuata njia ya msalaba.

Roho Mtakatifu daima atakuwepo kutusaidia anapoona dhamira yetu ya kuyashinda majaribu na kuzipinga tamaa za miili yetu. Hapa ndipo neema ya Mungu, uweza wake wa Uungu, unapoingilia kati. Haimaanishi kwamba anadhibiti kila kitu, kwani sisi daima tutakuwa na nafasi yetu katika kuzipinga tamaa za miili yetu. Roho hufanya kazi ndani yetu ili tusishindwe na majaribu, na shauku yetu na udhibitifu wetu katika kumtii hutuwezesha kuupata ushindi. Hakika, kujikana sisi wenyewe kwa msaada wa neema ya Mungu ndiyo njia ya Mungu ya kuyakimbia majaribu. Msalaba ndio unaoleta ushindi dhidi ya majaribu (na kwa maana hiyo dhidi ya dhambi). Huu ushindi nao hutuwezesha kukua na kuudhihirisha uhai wa Kristo.

Paulo analithibitisha hili katika waraka wake kwa Warumi 8:12, anaposema, *“…tu wadeni, si wa mwili”*, akimaanisha hatuna deni kwa mwili, na kwa hivyo hatulazimiki kuutii.

Hakika, sio kila wakati tunafanikiwa, lakini Bwana huiona shauku yetu ya kutaka kuenenda katika utakatifu nyakati tunapoanguka, lakini tukizitubia dhambi zetu kwa moyo wa dhati, Roho Mtakatifu hutusaidia kusimama tena na kurejea kwenye njia inayoelekea kwenye ushindi. Mwisho wa siku, jumla ya haya mambo yote ni ili kutuwezesha kukua kiroho, makusudi tuzidi kufanana na Kristo.

## Majaribu na Shetani

Kuna upande mwingine muhimu wa majaribu ambao ningependa kuutaja. Jaribu mara nyingi huja moja kwa moja kutoka kwa shetani, ambaye hutaka tufanye maamuzi yasiyokuwa na faida kwetu na yaliyo kinyume na mapenzi ya Mungu. Kwa mfano, anaweza kutujaribu kuikubali kazi ambayo itakuwa na madhara kwetu kiroho. Ibilisi ni mwongo na hulenga katika kutudanganya tuamini jambo fulani ni zuri kwetu wakati sivyo. Mara nyingi, atajaribu hata kutupofusha kwa kuileta mipango yake ionekane kama ni baraka kutoka kwa Mungu makusudi tuikubali na tuvutwe tumuache Bwana. Uongo wa jinsi hiyo kutoka kwa adui mara nyingi hufanya kazi dhidi yetu kwa kuzishawishi tamaa za miili yetu. Shetani hatatuonya kamwe juu ya mitego iliyoko mbele yetu, na ni katika nyakati kama hizi tunapotakiwa kuzinyamazisha tamaa za miili yetu na kuisikiliza sauti ya Roho Mtakatifu. Kumbuka kwamba si kila mlango unaofunguka mbele yetu unaotoka kwa Bwana, na kwa hivyo ni wajibu wetu kutambua ni kipi kinachotoka kwake na kipi hakitoki kwake.

Maadam tuko katika miili hii, tutaendelea kukutana na majaribu, lakini njia pekee ya ushindi daima itabaki ni katika kuuchukua msalaba wetu!

### Sura ya IX

# Ushindi na Msalaba

Tunaweza kuwa na kazi nzuri, sifa nzuri, pesa nyingi, matarajio yaliyotimia na kila hitaji likiwa limetimizwa vizuri maishani mwetu, bali kwetu sisi Wakristo, mafanikio ya kweli ni kuwa na ushindi juu ya dhambi.

## Utakaso: Lengo la Mkristo

Yesu anatuagiza: *“Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.”* (Mathayo 5:48). Mtume Paulo pia anatuhimiza: *“Basi, dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake.”* (Warumi 6:12). Na katika 1 Wathesalonike 4:3-4, anathibitisha kwamba mapenzi ya Mungu kwetu ni kutakaswa kwetu. Kwa Wakristo wengi,

kuyaishi haya maisha linaonekana ni jambo lisilowezekana. Lakini mpango wa Mungu si tu kutusamehe dhambi zetu, bali pia ni kuona tukienenda katika ushindi dhidi ya dhambi tuwapo hapa duniani. Hili linatuhakikishia ya kwamba yeye pia atatuwezesha kulifikia hilo lengo... hata kama hatutalifikia kwa siku moja.

Katika Warumi 7:21-25, Paulo anazungumzia vita inayoendelea ndani yake - zile sheria mbili zinazopingana katika utendaji. Sheria ya kwanza inatokana na dhambi iliyomo katika viungo vya mwili wake na nyingine inatoka kwa Mungu. Anamshukuru Mungu kwa ajili ya ushindi anaotupatia kwani anatambua ya kwamba sheria ya Roho wa uzima ulio katika Kristo Yesu imemweka huru mbali na sheria ya dhambi na mauti (Warumi 8:1-2). Kwake yeye, ushindi wa kweli ni ule upatikanao dhidi ya dhambi.

Tunafahamu ya kwamba Kristo aliishinda dhambi kama mwanadamu, kwa kuishi maisha makamilifu. Aliishi katika mwili ule ule tulio nao na alijaribiwa kama sisi nasi tujaribiwavyo. Hata hivyo, kwa kuwa hakuirithi asili ya dhambi kutoka kwa Adamu, na kwa kuwa hakushindwa na dhambi, aliweza kuichukua dhambi ya wanadamu wote katika nafsi yake alipokufa msalabani. Ushindi wake juu ya dhambi ulimruhusu Mungu, Baba, kumfufua kutoka kwa wafu. Ushindi huu wa kipekee unatutia moyo, kwa sababu unaimarisha imani yetu na kutuhakikishia ya kwamba tunapotembea katika kuzifuata nyayo za Yesu, tutaweza kuyafikia maisha matakatifu.

## Ushindi juu ya dhambi chini ya Agano Jipya

Paulo anaendelea kusema: *“Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi, kwa sababu hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema.”* (Warumi 6:14).

Kwa kuwa hatuko tena chini ya Sheria ya Musa, hatuhukumiwi kwa sababu ya dhambi zetu. Hata hivyo, hilo halimaanishi tuiache dhambi itutawale. Hatupaswi kusahau ya kwamba Yesu alipata ushindi dhidi ya dhambi ili kwamba sisi nasi tupate ushindi huo huo pamoja na furaha ya kuzidi kuwekwa huru mbali na dhambi. Hatukuitwa tuendelee kuwa watumwa wa dhambi bali watumwa wa Kristo.

## Ushindi upatikanao msalabani

Ushindi huu unatokana na namna tulivyo tayari kuuchukua msalaba wetu na kumfuata Yesu. *“Basi kwa kuwa Kristo aliteswa katika mwili wake, ninyi nanyi jivikeni silaha ya nia ile ile; kwa maana yeye aliyeteswa katika mwili ameachana na dhambi. Tangu sasa msiendelee kuishi katika tamaa za wanadamu, bali katika mapenzi ya Mungu, wakati wenu uliobaki wa kukaa hapa duniani.”* (1 Petro 4:1-2).

Hapa, Mtume Petro anaeleza wazi ya kwamba ikiwa tunataka ushindi juu ya dhambi, basi tunahitajika kuisulubisha miili yetu. Anasihi tuwe na hali ya moyo aliyokuwa nayo Yesu alipouendea msalaba na tujivike nia ile ile aliyokuwa nayo. Ushindi huu unakuwa wetu kwa kadiri tulivyo tayari kumtii Roho, na si miili yetu.

Mtume Paulo anasema jambo lilo hilo katika Wagalatia 5:24: *“Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulibisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake.”*

Kwa maana hiyo, hakuna njia elfu za ushindi juu ya dhambi, ni moja tu: kuyafananisha maisha yetu na Kristo na kuuchukua msalaba wetu. Bila shaka ingekuwa rahisi zaidi tungetakiwa tu kusali sala fupi... lakini kuuchukua msalaba wetu ndiyo njia pekee ya ushindi.

Ushindi juu ya dhambi hufungua mlango kwa ajili ya kupata ushindi katika mambo mengine pamoja na baraka maishani mwetu, kwa sababu Mungu huwapa thawabu wale walio tayari kuuchukua msalaba wao na kumfuata.

## Sura ya X

# Mateso na Msalaba

Maisha ya Ukristo ni mchanganyiko wa furaha, huzuni, shangwe, machozi, wingi, kupungukiwa, mateso, baraka, na ushindi. Vyovyote tutakavyolitazama hili, tumeitwa kuteseka kwa ajili ya injili, bila kuhesabu idadi ya majaribu ambayo tutalazimika kuyapitia maishani mwetu.

## Kuteseka kwa ajili ya injili

Hatuna budi kukutana na udhia tunapoitangaza na kuitetea injili ya kweli. Hakuna jambo la ajabu katika hilo na hatupaswi kushtushwa nalo. Yesu mwenyewe alisema, *"…Mtumwa si mkubwa kuliko bwana wake. Ikiwa waliniudhi mimi, watawaudhi ninyi..."* (Yohana 15:20).

Ujumbe aliohubiri Yesu pamoja na mitume wa kwanza sikuzote uliambatana na ahadi ya kuudhiwa. Hii ndio sababu wale wanaoihubiri injili na hawakabiliani na ushindani wa aina yoyote wanapaswa wajihoji kama wanaihubiri injili ya kweli. Tuko katikati ya vita ya kiroho na tunapaswa kutarajia upinzani. Ikiwa kila mtu anafurahia kusikiliza kile sisi wachungaji tunachohubiri, basi tunapaswa tujiangalie upya. Vivyo hivyo, Mkristo ambaye maisha yake yametiishwa kwa Kristo hawezi kutarajia kukubalika na kila mtu.

*"Maana mmepewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, ila na kuteswa kwa ajili yake..."* (Wafilipi 1:29). Mtume Paulo aliteswa visivyo haki kwa ajili ya injili, lakini alifahamu ilikuwa ni sehemu ya wito wa Mungu juu ya maisha yake na ya kwamba neema ya Mungu ingekuwepo kumsaidia katika kila jambo. Sababu iliyomfanya asilaumu ni kwa kuwa aliupata ufunuo wa injili ya Kristo.

Ni lazima tuelewe ya kwamba sisi kama Wakristo tuko katika vita ya kiroho. Paulo alifahamu, kwa mfano, ya kwamba aliwekwa gerezani kutokana na hilo. Hakujaribu kuwaza akilini mwake ni kwa nini hili limemtokea. Alielewa kulikuwa na vita inayoendelea kati ya nuru na giza na ya kwamba

kuteseka kwa ajili ya kweli na haki ni jambo la kawaida kwa Mkristo yeyote anayemtumikia Bwana.

Paulo alikuwa na wapinzani wengi waliomwinukia kwa sababu walikataa kuichukua changamoto iliyoletwa na injili. Aliwaonya hata Wafilipi dhidi ya wale wanaoenenda kama maadui wa msalaba wa Kristo (Wafilipi 3:18).

Hata hivyo, jambo la muhimu kuzingatia ni kwamba hakubeba lawama yoyote, na wala hakuwa na uchungu nao. Kinyume chake alijivunia na kuhisi amejaliwa heshima kuweza kuitangaza kweli ya injili, ujumbe wa msalaba, huku akiteswa kwa ajili yake.

Maadui zake walizitumia shida na mateso yake kujaribu kuwavunja moyo Wakristo kutoufuata mfano wake na kuwageuza wasiyafuate maisha halisi ya Ukristo. Walitaka kuonyesha ya kwamba udhaifu wa Paulo - majaribu na adha alizokutana nazo - yalikuwa ni ushahidi ya kwamba injili yake haikuwa na nguvu. Walichokosa kukiona ni kwamba ukweli ulikuwa kinyume: maisha ya Paulo yalikuwa ni matunda na kielelezo cha ujumbe aliouhubiri na kuuishi. Walichagua kumpinga kuliko kukubali kumulikwa na kweli ya injili na kumruhusu Mungu awabadilishe katika mfano wa Kristo.

*"Maana, alisulibiwa katika udhaifu, lakini anaishi kwa nguvu za Mungu. Maana sisi nasi tu dhaifu katika yeye; lakini tutaishi pamoja naye kwa uweza wa Mungu ulio kwenu."* (2 Wakorintho 13:4). Wakorintho walikuwa wakitafuta ushahidi ya kuwa Kristo alinena kupitia Mtume Paulo. Walifahamu ya kuwa Yesu alikuwa na uwezo, lakini walipoyaangalia maisha ya Paulo, yalionekana kinyume. Lakini Paulo alitaka waelewe ya kuwa ingawa Yesu aliudhihirisha uwezo wake wakati alipokuwa duniani, bali hakupigana alipopelekwa msalabani, alionekana dhaifu na asiye na nguvu. Kwa maana hiyo alichukua kielelezo cha udhaifu wa Yesu maishani mwake, akiwa tayari kujinyenyekeza kwa njia ile ile na akiwa tayari kuteseka ili mpango wa Mungu utimizwe.

Yesu aliyasalimisha mamlaka yake na akakubali kupoteza kila kitu kwa ajili ya mapenzi na mpango wa Baba yake. Vivyo hivyo, Paulo alikubali kuteseka kwa ajili ya Kristo na kukabiliana na majaribu na adha katika huduma yake, huku akijua ya kwamba nguvu ya Mungu na uzima wa Yesu vingefunuliwa kutokana na utumishi wake kwa Kanisa.

Si wote tunaopata adha kama wale wanaouawa kwa ajili ya imani yao katika baadhi ya nchi. Lakini tunaposhitakiwa isivyo haki na kushambuliwa kwa ajili tu ya imani yetu katika Bwana, na kwa ajili ya msimamo wetu katika injili, hili pia linaweza kuhesabiwa kama kuudhiwa kwa ajili ya injili.

Miaka kadhaa iliyopita, familia yangu pamoja na kanisa letu tulipitia wakati mgumu sana tuliposhambuliwa kwa mashtaka ya uongo yaliyochapishwa kwenye vichwa vya habari magazetini kwa wiki kadhaa. Mimi pamoja na mke wangu ndio tulikuwa tumeanza kuielewa injili ya msalaba kwa hivyo hili lilikuwa ni jaribu kubwa la imani yetu, na ulikuwa ni wakati wa kuenenda katika nuru tuliyokuwa tumeipokea. Tungeweza kuchagua kujitetea kwa kujibu yale mashtaka au kunyamaza, na kuwasamehe waliotunena vibaya, kuwaombea, na kumwekea Bwana tumaini letu. Kwa neema ya Mungu tuliweza kuchagua hili la pili.

Ulikuwa ni wakati mgumu sana, lakini Mungu alikuwa mwaminifu hadi mwisho na tulitoka katika lile jaribu tukiwa tumebadilika na kukomaa ki-imani. Ninapolitafakari, ninambariki Bwana kwa nyakati hizo kwa sababu ninaamini kwa nguvu zangu zote ya kuwa mambo makubwa yanayofanyika kanisani kwetu leo hii kwa sehemu yametokana na uamuzi tuliochukua wa kuifuata njia ya msalaba tulipojaribiwa. Mungu anajua namna ya kuwazawadia watoto wake; yeye ni mwaminifu!

Kama Mtume Petro asemavyo, *“Wapenzi, msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho,”* (1 Petro 4:12), na katika msitari unaofuata, *“...furahini; ili na katika ufunuo wa utukufu wake mfurahi kwa shangwe.”* Tunaposoma haya, tunaona ya kuwa adha ni jambo la kawaida kwa Mkristo, na nyakati kama hizo zinakuwa ndizo nyakati tulizoitwa kuuchukua msalaba wetu na kujifananisha na Yesu.

Ni wazi, kama Petro anavyosisitiza, ya kwamba tunapoteseka, isiwe ni kwa sababu tumetenda mabaya! Hili likitokea, itakuwa ni matunda tu ya matendo yetu maovu. (1 Petro 4:15).

Mtume Yakobo pia anazungumzia mateso: *“Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno.”* (Yakobo 1:2-4).

Anatusaidia kuelewa ya kwamba majaribu mbalimbali tunayokutana nayo yapo ili kutukamilisha na kuiimarisha imani yetu. Kumbuka ya kuwa tuko kwenye mbio za ukamilifu.

Kama tulivyoona awali katika 2 Wakorintho 12:7-9, Paulo anazungumzia 'mwiba katika mwili' ambao alimuomba Mungu amuondolee, lakini jibu la Mungu lilikuwa wazi: *"...Neema yangu yakutosha..."* Katika msitari wa 10, anaelezea hivi, *"Kwa hiyo napendezwa na udhaifu... ndipo nilipo na nguvu."* Ni wazi ya kwamba alikuwa na ahadi na uhakika ya kwamba neema ya Mungu ingefunuliwa katika udhaifu. Huyo ni mtumishi wa Mungu anayefurahia kumtumikia Yesu katika hali yoyote ile!

## Majaribu ya maisha

Ni muhimu kwetu kuelewa ya kuwa, kama Wakristo, tutapitia aina nyingi za majaribu maishani mwetu. Yanaweza kuwa ni ya kimwili au ya ki-mawazo: ugonjwa, kudhulumiwa haki zetu kazini, matatizo ya kiuchumi, kukosa kazi, ukiwa, kukataliwa na waume zetu au wake zetu, masuala ya kifamilia... orodha ni ndefu. Hata hivyo, hatupaswi kukata tamaa nyakati kama hizo. Tunapaswa kuwa na uhakika ya kwamba Mungu hajatusahau na ya kwamba anajua vema namna ya kutufariji na kutuinua. Neema yake daima ipo kwa ajili ya kutuwezesha kusonga mbele.

Jambo baya zaidi tunaloweza kufanya ni kujilinganisha na watu wengine au kujaribu kuwaza akilini mwetu ni kwa nini tunapitia yale tunayoyapitia. Hiyo njia inaweza kutufanya tuusahau upendo na uaminifu wa Mungu kwetu na inaweza hata kutusababisha kumnung'unikia.

Hebu angalia kile Paulo anachotuambia katika 2 Wakorintho 4:17-18: *"Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele."* Je! haya maandiko yanatutia moyo kiasi gani tunapoamua kuyazingatia! Na hii ndiyo njia pekee tutakayoweza kuing'ang'ania neema ya Mungu, kwani hakuna kitu kinachoweza kututenga na upendo wake. (Warumi 8:35).

Hebu tuibebe nia ile ile na tumaini lile lile alilokuwa nalo Paulo katika majaribu na mateso yetu, na tuyapitie katika roho sahihi, huku tukijua ya kwamba tuna taraja katika Bwana kwa njia ya imani.

## Sura ya XI

# Imani na Msalaba

Imani ni kitu muhimu katika maisha ya Mkristo. Katika Waebrania 11:6, mwandishi anatuambia waziwazi ya kwamba pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu. Anatufundisha pia ya kwamba mwenye haki ataishi kwa imani: huu ndio mtindo mpya wa maisha kwa kila Mkristo (Waebrania 10:38). Kila kitu tunachotazamia kutoka kwa Bwana, kila kitu tunachotafuta, tunachotamani, au tunachotarajia kuwa, ni lazima kipokelewe kwa imani.

## Kuutafuta Ufalme wa Mungu

Wakristo mara nyingi huiona imani kama njia ya kujipatia 'wanachohitaji', au wanachotaka. Hawatambui ya kwamba wanapoifanyia kazi imani yao, Bwana anaweza kuwapitisha katika jaribu ili wazidi kufanana na Kristo. Imani kazi yake ya kwanza ni kutusaidia kukua kiroho.

Kwa bahati mbaya, Kanisa halijafanikiwa kuwafundisha watu wa Mungu hili. Kwa Wakristo wengi, imani inatumika tu kama njia ya kujitafutia mahitaji yao ya kimwili, kana kwamba hilo ndilo kusudi kuu la Mungu... Leo hii mkazo unawekewa mambo ya maisha haya, huku Wakristo wakivutwa kutoka katika kutafuta kile ambacho ndicho kinapaswa kuwa kipaumbele chao: Ufalme wa Mungu. Bwana mwenyewe anasema: *"Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa."* (Mathayo 6:33).

## Imani kwa ajili ya urithi wetu

Kitabu cha Waebrania kinatuonyesha ya kwamba sababu kuu mojawapo ya Bwana kutupatia imani ni ili tuwe na uhakika wa urithi wetu wa milele ulioahidiwa kwa wale walioitwa. (Waebrania 9:15).

Waebrania 10:35-36 inatutia moyo, *"...msiutupe ujasiri wenu, kwa maana una thawabu kuu. Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi."* Tumepewa imani ili tuweze kuikazia

macho ahadi ya utukufu ujao. Tunatiwa moyo kustahimili katika hiyo imani huku tukimsubiri Yesu arudi. Imani inayozungumziwa hapa si kwa ajili ya mali ya dunia hii au vitu vya muda tu bali kinyume chake, ni imani kwa ajili ya kutuwezesha kuishikilia ahadi yetu, ya kwamba tutaishi milele na Yesu.

Tena na tena, tunajikuta tukitiwa moyo tusikate tamaa bali tudumu katika imani: *"Lakini sisi hatumo miongoni mwao wasitao na kupotea, bali tumo miongoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu."* (Waebrania 10:39). Huu msitari unasisitiza tena kazi ya imani kuwa ni kutuandaa kwa ajili ya unyakuo wa Kanisa. Hii ni changamoto kubwa kwa watu wa Mungu!

## Imani kupitia majaribu

*"Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno."* (Yakobo 1:2-4). Kama tulivyokwisha kusema, kustahimili katika imani, kama Mtume Yakobo anavyozungumza hapa, hutuandaa kwa ajili ya kustahimili majaribu, dhiki, adha na mateso. Anatuonyesha ya kwamba ni jambo la kawaida kwetu kupitia dhiki za aina hiyo, na hata kwamba hili ni muhimu kwa ajili ya kukua kiroho. Lakini mara nyingi, Wakristo hawako tayari kuyakubali majaribu kama hayo kwa sababu wanafikiria Mkristo hapaswi kupitia mambo ya jinsi hiyo. Kutokana na tafsiri potofu ya kile maisha ya Ukristo na injili yanapaswa kuwa, hili linawaacha wengi wakiwa wamekata tamaa huku wakijaribu kila njia ili kuzikwepa dhiki na changamoto. Wengine, kwa mfano, wanageukia kukemea pepo, huku wakiamini ya kuwa mapepo ndio chanzo cha matatizo yao. Wengine wanageukia maombezi kanisani kwa kuamini ya kwamba mtu akiwaombea, tatizo litaondoka lenyewe. Lakini tunachofanya hapo ni kutafuta njia rahisi za kusuluhisha shida na matatizo, ilhali tumeitwa tukubali kuzipitia hali hizi hizi kwa sababu nzuri sana: imani yetu ni sharti ijaribiwe ili tuweze kuufikia utu uzima rohoni.

## Saburi: matokeo ya imani iliyojaribiwa

Tukiangalia Yakobo 1:3 kwa umakini, tutaona ya kwamba kujaribiwa kwa imani yetu huleta saburi, ambalo ni tunda mojawapo la imani. (Wagalatia 5:22). Ingekuwa imani yetu haijaribiwi, tusingekuwa na haja ya

kuwa na saburi. Mkristo anapoomba jambo ambalo lipo katika mapenzi ya Mungu na asipokee majibu ya papo kwa papo (na hili hutokea mara nyingi sana), hapo ndipo anapotakiwa kuwa na subira. Muda huo ndipo imani yake inapokuwa ikijaribiwa. Anahitajika amsubiri Bwana, na asiwe na shaka yoyote, ikiwa anataka kupokea kile alichokiomba, na akabiliane na hizi nyakati kwa matumiani moyoni mwake, kwa kuwa haiwezekani tumaini liwepo bila imani. Hebu tuchukue mfano wa mume na mke, kwa mfano. Mara nyingi tunapenda kuona maeneo fulani fulani katika maisha ya mwenza wetu yakibadilika haraka na kwa kiasi kikubwa kwa sababu hatuko tayari kuwakubali kama walivyo. Ila ikiwa tunaamini Mungu anaweza kuwabadilisha basi itabidi tuwe wavumilivu na tumngoje Bwana afanye.

Inahitajika kazi ya Bwana ili kila mmoja wetu aweze kumkubali mwenzake kama alivyo, huku kila mtu akizidi kumwamini Mungu kwa ajili ya mwenzake, na kwa ajili yake mwenyewe, katika kupata badiliko! Hapa ndipo kila mmoja wetu anapopaswa kuuchukua msalaba wake. Tunapokuwa tukilisubiri hili badiliko, imani yetu itajaribiwa, lakini tukidumu katika imani na kuzishinda hali zetu za kimwili katika kutokuibeba hali mbaya ya moyo kwa wenza wetu, tutakua rohoni.

Hata katika Agano la Kale tunaona jinsi Mungu alivyowajaribu wana wa Israeli: *"Nawe utaikumbuka njia ile yote Bwana, Mungu wako aliyokuongoza miaka hii arobaini katika jangwa, ili akutweze, kukujaribu kuyajua yaliyo moyoni mwako, kwamba utashika amri zake, au sivyo."* (Kumbukumbu la Torati 8:2). Muda wao wa kukaa jangwani haukukosa majaribu na mateso, lakini ulimpa nafasi Mungu kuwajaribu watu wake.

Katika kila kitu tunachoomba au kupokea kwa imani, ikiwemo mali ya dunia hii, Mungu anataka kujenga jambo la rohoni maishani mwetu. Tukiuondoa msalaba katika imani yetu, tunaiondolea imani nguvu yake, na kuifanya kuwa chombo cha kupokea mambo tu tunayotaka kutoka kwa Mungu. Lakini imani ni kiungo muhimu katika safari yetu ya rohoni: katika kupokea kile Mungu alichonacho kwa ajili yetu, imani humruhusu Mungu kutenda kazi maishani mwetu wakati huo, ili tuweze kumwakilisha vema zaidi, kumtumikia vema zaidi na, zaidi ya yote, kuumaliza mwendo.

## Sura ya XII

# Ukomavu wa kiroho na Msalaba

*“Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu, kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe, hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo.”* (Waefeso 4:11-13).

Utu uzima rohoni, au ukuaji wa kiroho, ni eneo mojawapo la maisha ya Kikristo ambalo limetajwa zaidi na Yesu na mitume katika Agano Jipya. Fundisho la Yesu linatuhimiza hasa kuishi maisha safi na matakatifu. Nyaraka zote za Mtume Paulo zinatuelekeza tuzidi kufanana na Yesu ili tuuwasilishe uhai wake kwa kadiri tunavyomtumikia.

Katika waraka wake kwa Wakolosai, Paulo anaelezea shauku yake ya kutaka kuwaona Wakolosai wakienenda katika kuuelekea ukamilifu: *“ambaye sisi tunamhubiri habari zake tukimwonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu katika hekima yote, tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo. Nami najitaabisha kwa neno lilo hilo, nikijitahidi kwa kadiri ya kutenda kazi kwake atendaye kazi ndani yangu kwa nguvu.”* (Wakolosai 1:28-29).

## Msalaba: njia ya kuufikia utu uzima rohoni

Basi tutafanyikaje watu wazima rohoni? Katika Mathayo 16:24, Yesu anawahimiza wanafunzi wake kujikana wenyewe, kuuchukua msalaba wao na kumfuata. Anawaonyesha wanachohitaji kufanya ili kukua kiroho na kuwa watakatifu. Bwana hajatuchagulia tukue kiroho kwa maarifa ya kichwani wala masomo ya kitheolojia. Mojawapo ya makosa makubwa ambayo Kanisa limeyafanya ni kujaribu kuwafanya wanaume na wanawake kuwa watu wa rohoni kwa njia ya mafundisho ya Biblia na mahudhurio katika shule za kibiblia. Ni wazi kwamba kujifunza Biblia ni muhimu, lakini

hili haliwezi kuchukua nafasi ya kuifuata njia ya msalaba katika kutufikisha katika utu uzima rohoni.

Katika sura ya 5 hadi ya 7 ya kitabu cha Mathayo, Yesu anatufundisha mtindo mpya wa maisha, ambapo tunahitajika tuzifie nafsi zetu na kuzikana haki zetu. Badala ya kuwachukia adui zetu, kwa mfano, anatuagiza tuwapende. Nina hakika utakubali kuwa hili ni kinyume kabisa na matakwa yetu ya asili, ya kimwili!

Kukubali kuutoa uhai wetu na kuweka kando asili zetu za zamani ndiyo njia pekee ya kuyaishi maisha ya ushindi na utakatifu. Sisi kama Wakristo tumeitwa tuisulubishe miili yetu pamoja na tamaa zake na shauku zake, kama Paulo anavyotukumbusha katika Wagalatia 5:24. Hili ndilo linalotufanya tuzidi kufanana na Kristo na kuubeba uhai wake. (Wagalatia 2:20). Mwisho wa siku, njia pekee ya kuufikia utu uzima rohoni ni kuwa tayari kupoteza maisha yako ili uyapate ya Kristo.

## Kuifia nafsi ili kuzaa matunda

Yesu alitumia mfano wa chembe ya ngano inapoanguka ardhini na kufa katika kutuonyesha uhai unaotoka kwetu tunapoamua kuzifia nafsi zetu. Baada ya kutangaza ya kuwa wakati wa kutukuzwa kwake ulikuwa umewadia, aliwaambia wanafunzi wake, *“Amin, amin, nawaambia, chembe ya ngano isipoanguka katika nchi, ikafa, hukaa hali iyo hiyo peke yake; bali ikifa, hutoa mazao mengi.”* (Yohana 12:24). Yesu alikuwa hazungumzi tu kwa habari ya kifo chake na kufufuka kwake bali alikuwa akizungumzia pia maisha ya wanafunzi wake baada ya kufufuka kwake. Njia pekee ya kuubeba uhai wa Yesu ilikuwa ni kuuchukua msalaba wao. Msalaba unamaanisha kuzifia tamaa zetu za kimwili, shauku zetu, mipango yetu na matamanio yetu. Ni kuyaachilia maisha yetu ili tuyabebe ya Kristo, kwani ikiwa tutayashiriki maisha yake ya ufufuo, tutalazimika kwanza kushiriki katika mauti yake kwa kuzifia nafsi zetu.

Kama tulivyoona, sote tumeitwa tuyapitie majaribu, mateso, na shida katika maisha yetu ya Ukristo. Kutakuwa na changamoto, mateso, adha na upinzani maishani mwetu. Namna tutakavyokabiliana na hali hizi mbalimbali ndiyo itakayoamua ikiwa tutakua rohoni, au tutabaki wachanga rohoni. Ikiwa tuko tayari kuuchukua msalaba wetu na kukubali kuyapitia haya yote kwa

imani, basi Mungu ataweza kutuvunja na kututengeneza. Maisha ya jinsi hii yatasababisha uhai wa Yesu kufunuliwa ndani mwetu.

Nabii Yeremia alipokea maono ya kazi ya ndani ambayo Bwana anatamani kufanya maishani mwetu ili kutuumba kwa mfano wake: *"Ndipo neno la Bwana likanijia, kusema: Ee nyumba ya Israeli, je! Siwezi mimi kuwatendea ninyi vile vile kama mfinyanzi huyu alivyotenda? Asema Bwana. Angalieni, kama udongo ulivyo katika mkono wa mfinyanzi, ndivyo mlivyo ninyi katika mkono wangu, ee nyumba ya Israeli!"* (Yeremia 18:5-6). Maadam mfinyanzi hajaridhika na kazi yake, ataendelea kukifinyanga chombo hadi atakapofikia matokeo anayoyataka yeye. Swali ni: Je! tuko tayari kumruhusu Mungu afanye vivyo hivyo maishani mwetu?

Mara kwa mara tunakutana na kutofautiana au kukabiliana na migogoro katika maisha yetu ya kila siku, iwe ni kutoka kwa mume au mke wako, jamaa zako au marafiki zako. Haya yanapotokea, ni rahisi zaidi kutaka kujihesabia haki. Lakini hata kama tuko sahihi tunapaswa kujifunza kukubali kupoteza badala ya kujaribu kujilinda au kujitetea. Yesu alionyesha mfano huu huu, na ukomavu wa jinsi hii ndio tunaoitiwa tuulenge sisi kama Wakristo.

Namfahamu mchungaji mmoja barani Afrika aliyekuwa kiongozi msaidizi katika kanisa moja. Kila kitu kilichokuwa mle kanisani kilikuwa ni mali yake pamoja na kiongozi mwenzake: viti, vyombo vya sauti, gari la kanisa, n.k. Wakati ulifika ambapo wachungaji hawa wawili walishindwa kuelewana, na hivyo wakaamua kuachana. Lakini walipofikia namna ya kugawana ile mali, walishindwa kupatana. Hakuna aliyekuwa tayari kupoteza na mambo yakawa machungu kati yao. Wakati huo ndipo nilipokutana na huyu mchungaji kwa mara ya kwanza na kumshirikisha Mathayo 16:24; andiko ambalo bila shaka alilifahamu vizuri sana. Licha ya kwamba alikuwa mchungaji wa miaka mingi, hakuwahi kuelewa kina cha andiko hili, wala kuutambua umakini ambao lilihitaji kuchukuliwa nao. Nilimtia moyo kujikana nafsi na kuachilia haki zake. Baada ya kusita sita sana, mwishowe alikubali. Badala ya kupigana na mchungaji mwenzake, alikubali kuondoka na kumwachia kila kitu. Ingawa lilikuwa ni jambo gumu, lakini kupitia hilo alifikia kuielewa maana ya kuuchukua msalaba wake. Alipoteza kila kitu alichokuwa amewekeza katika lile kanisa lakini alibaki na amani na furaha nyingi kwa kuwa ameweza kujifananisha na Yesu kwa njia hii. Unapopoteza kitu kwa ajili ya Kristo, kwa sababu umeelewa wito wa kuuchukua msalaba wako, kuna mambo makubwa zaidi ambayo yanakungojea. Leo hii mchungaji huyu anamtumikia

Bwana, akiongoza idadi kubwa ya makanisa, akihubiri injili na kutumiwa na Bwana kwa namna ya kipekee barani kote Afrika. Ikiwa tunataka kukua katika Kristo basi hakuna kuukwepa msalaba; ni lazima kuyatoa maisha yetu na kuyaweka madhabahuni.

Mtume Paulo alijitahidi kumleta kila mtu mkamilifu katika Kristo, kwa maneno mengine mtu mzima rohoni, sio tu anayeyaelewa mambo ya rohoni bali anayeyaishi pia. Tuko katika mbio kuuelekea ukamilifu ingawa hakuna mtu aliye mkamilifu au atakayekuwa mkamilifu tukiwa tungali bado duniani. Tunaweza tu kuendelea kukua hatua kwa hatua na kuzidi kufanana na Yesu, jambo ambalo linawezekana kabisa ikiwa tutajisalimisha kwake, tukiwa tayari kujinyenyekeza na kuuchukua msalaba wetu. Kwa kufanya hivyo, Mkristo anayaweka maisha yake mikononi mwa Bwana, ambaye ndiye anayejua jinsi ya kuimaliza kazi aliyioanza maishani mwa mtu. Na hakika, Paulo hata anasema ya kwamba, *"Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu."* (Wafilipi 1:6).

## Msalaba: changamoto kwa Wakristo leo

Kabla ya kufahamu ufunuo wa ujumbe wa msalaba, kanisa nililokuwa ninachunga lilikuwa linakabiliwa na matatizo mengi ambayo hapakuwepo na matumaini yoyote ya kuyatatua. Ijapokuwa Neno la Mungu halikuacha kuhubiriwa, wanandoa wengi waliendelea kuachana, dhambi ilishamiri, na vijana walikuwa wakivutwa sana na dunia na mambo yake. Mara tu ujumbe wa msalaba ulipofunuliwa katika mioyo yetu, wazee wa kanisa na mimi mwenyewe tulishuhudia mabadiliko makubwa na ujumbe huu uliyagusa maisha ya wengine wengi mle kanisani. Sote tulipitia kipindi cha toba ya kweli. Hali ya hewa rohoni ilibadilika na wengi walishuhudia ukuaji mkubwa wa kiroho. Bado hatujafikia ukamilifu! Lakini kila mtu amekua na ameimarishwa katika Yesu, sote tukizidi kuwa na bidii ya kuupitia mlango mwembamba. Thawabu yetu kubwa leo ni kuuona umoja unaolitawala kanisa letu.

Nakumbuka niliwahi kumtembelea mchungaji mmoja wa kanisa la kipentekoste nchini Marekani miaka kadhaa iliyopita. Katika mazungumzo yetu, nilimweleza ya kwamba ujumbe wa msalaba ndilo jawabu kwa kanisa. Nilimwambia ya kwamba Wakristo hawakuitwa wafukuzane na mali ya dunia hii au mambo yao binafsi, bali wameitwa wayapoteze maisha yao,

wauchukue msalaba wao na kumfuata Yesu na ya kwamba hii ndiyo njia ya kufanyika mtu mzima na kupata ushindi rohoni. Akanijibu kwa utulivu kabisa, *"Ninakubaliana kabisa na wewe, lakini kama nitahubiri ujumbe huo, nitapoteza idadi kubwa ya washirika wangu."* Nilishtushwa sana na jibu lake, na nikatambua kwa huzuni ya kuwa hili kanisa lilikuwa masikini sana kiroho. Katika hali kama hizi, haishangazi kuona kwamba Wakristo wengi bado ni watoto wachanga kiroho, wanaotupwa huku na huko na kila upepo wa mafundisho, na hawana uwezo wa kutambua mambo ya Roho.

Kanisa la leo linapata shida kubwa katika kuwafanya Wakristo kuwa wanafunzi wa kweli wa Kristo, ambao wamejitolea kuzikimbia mbio ambamo maisha yao sio yao tena. Ukuaji wa kiroho hauwavutii. Kuutoa uhai na kuuchukua msalaba ni changamoto kubwa sana kwao. Wanapendelea kuishi maisha ya 'kidini' ambayo hayatoi nafasi ya kukabiliwa kwa miili yao na kuleta haja ya mabadiliko. Lakini Yesu alikuwa wazi sana kuhusu eneo hili: *"Yeye aipendaye nafsi yake ataiangamiza; naye aichukiaye nafsi yake katika ulimwengu huu ataisalimisha hata uzima wa milele."* (Yohana 12:25).

Hata hivyo, ni kweli kwamba wengi hawajawahi kuusikia ujumbe kamili wa msalaba, unaoweza kuleta ukomavu maishani mwao. Licha ya upendo wao wa kweli kwa Bwana, lakini hawaendelei. Wanahudhuria ibada kwa uaminifu lakini hawasikii kitu kitakachowasaidia kukua kiroho. Wengi wamevunjika moyo kwa kuwa hawana ushindi katika maeneo fulani katika maisha yao. Upendo wao kwa Bwana unapoa na wakati mwingine hata wanakata tamaa. Hata hivyo hatuwezi kuwalaumu kwani hali yao inategemea chakula cha kiroho wanachopata kanisani. Katika hali hii ni kwa muujiza upi watakuwa watu wazima rohoni na si Wakristo wa mwilini?

Wakati fulani niliendesha kongamano la wachungaji barani Afrika ambapo nilihubiri juu ya ujumbe wa msalaba. Baada ya mahubiri ya siku ya kwanza, mchungaji mmoja mzee wa miaka 70 alikuja kuniona. Alikuwa na furaha isiyokuwa na kifani aliponiambia ya kuwa alikuwa hajausikia ujumbe wa jinsi hii kwa miaka mingi na ya kwamba haikumshangaza kuona kwamba makanisa nchini mwake yalikuwa yamegawanyika na hayakuwa na uhai tena. Nilitiwa moyo sana na kile alichokisema, kwani nilikuwa nimezoea kukutana na wachungaji ambao hawaukubali ujumbe wa msalaba, ama kwa kukosa ufunuo, au kwa sababu walihisi kukabiliwa na huu ujumbe na wakapendelea zaidi kuficha maeneo fulani ya maisha yao. Ujumbe wa msalaba sikuzote umekuwa ukipingwa na utaendelea kupingwa, hata kutoka ndani ya Kanisa.

Ila kwa wakati wake, Bwana anajua jinsi ya kufungua na kuigusa mioyo ya wale aliowakusudia waupate mwanga wa injili.

Huu ulikuwa ndio ujumbe wa kitume wa Kanisa la Kwanza, ambao ulihubiriwa upya kwenye karne ya ishirini katika miaka ya 1950 hadi 1960. Baadaye lilikuja wimbi la mafundisho ya mafanikio, ambayo yaliivuta mioyo ya wengi Kanisani katika kufukuzia mambo ya mwilini. Wahubiri na wachungaji wengi walivutwa na haya mafundisho potofu na wakaondoka kuyafuata wakiwa na idadi kubwa ya Wakristo. Hivi ndivyo, taratibu lakini kwa uhakika, ujumbe wa msalaba ulivyoondolewa katika mafundisho na mahubiri ya makanisa mengi. Hatupaswi kushangazwa, basi, kuona sehemu kubwa ya Kanisa likiwa dhaifu na likiwa imejawa na mafundisho potofu!

Mtume Paulo alifurahia kuuchukua msalaba wake. Alikuwa amewekwa huru mbali na vishawishi vya kidunia na alifanyika kielelezo cha ukomavu wa kiroho kutokana na namna alivyojifananisha na Kristo. Hii ndiyo maana aliweza kuwaambia Wafilipi wamfuate na kwamba wawaangalie wale walioenenda kwa kuufuata mfano waliowaachia. (Wafilipi 3:10-17). Katika kifungu kingine, anazungumzia jinsi Wafilipi walivyopewa neema ya Mungu, *"...si kumwamini tu, ila na kuteswa kwa ajili yake..."* (Wafilipi 1:29).

Katika kukubali kuifia nafsi na kuweka chini kila silaha, tunaruhusu kazi ya ndani ya Mungu yenye kututakasa na kuleta utu uzima wa kiroho maishani mwetu; hili ndilo tunda la Roho lililotajwa katika Wagalatia 5:22. Msalaba si tu tukio lililofanyika miaka 2000 iliyopita kwa ajili ya kutuokoa, bali ni jambo ambalo ni lazima lifanyike sehemu ya maisha yetu ya kila siku ikiwa tunatamani kukua kiroho.

## Sura ya XIII

# Uhuru na Msalaba

Kuna pande mbili katika uhuru wetu kama Wakristo. Kwa upande mmoja, tumewekwa huru mbali na dhambi iliyotuchukua mateka kwa muda mrefu kabla ya kuokolewa. Kwa upande mwingine, tuko huru kufanya maamuzi yetu wenyewe na kutenda sawa sawa na hayo maamuzi, kwa kuwa hatupo tena chini ya Torati ya Musa, bali chini ya neema. Maeneo haya mawili ya uhuru wetu yanaingiliana, kwani tunaweza kuwekwa huru mbali na dhambi chini ya neema tu.

## Kuongozwa na Roho Mtakatifu

Katika Warumi, Mtume Paulo analiambia Kanisa ya kwamba sasa wako huru katika Kristo: *"Bali sasa tumefunguliwa katika torati, tumeifia hali ile iliyotupinga, ili sisi tupate kutumika katika hali mpya ya roho, si katika hali ya zamani, ya andiko."* (Warumi 7:6). Analizungumzia jambo hilo hilo katika waraka wake kwa Wakolosai: *"... akiisha kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea msalabani."* (Wakolosai 2:14). Katika Wagalatia, anaendelea kwa kusema: *"Kristo alitukomboa katika laana ya torati..."* (Wagalatia 3:13).

Ni muhimu kuelewa ya kwamba Torati ilikuwa laana kwa maana ya kwamba iliambatana na hukumu. Aidha, isingeweza kutukamilisha na kutuweka huru kutokana na dhambi. Ikiwa tutachagua kubaki chini ya Sheria, hatuwezi kukua na kuufikia utu uzima rohoni. Tutabaki kuwa watumwa wa dhambi ile ile inayotuhukumu. Mwandishi wa Waebrania anatuambia ya kwamba, *"...Maana, kuna kubatiliwa kwa ile amri iliyotangulia", kwa maana nyingine, Sheria, "kwa sababu ya udhaifu wake, na kutokufaa kwake. kwa maana ile sheria haikukamilisha neno..."* (Waebrania 7:18-19).

Kwa hiyo, kama Wakristo walio chini ya Agano Jipya, hatukuitwa kuongozwa na Torati (au Sheria), bali tunaongozwa na Roho Mtakatifu ambaye ndiye

dira yetu na kiongozi wetu na ndiye anayetufundisha njia za Bwana. Roho Mtakatifu, ambaye amechukua nafasi ya Sheria, hutusaidia kufikia matakwa yake katika uhuru. (Warumi 8:4).

Paulo anapoandika, *"Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti,"* hapa anazungumzia Sheria ya Musa. (Warumi 8:2). Ingawa tumeitwa kumtii Roho Mtakatifu, daima tuna uhuru wa kutokufanya hivyo. Ni juu yetu, ni uchaguzi wetu kabisa; na hili linatokana na uhuru Kristo aliotupatia kupitia msalaba.

Kumtii Roho humaanisha kuifia nafsi; kuyakataa maisha yetu na tamaa zetu. Kumtii Kristo, basi, ni 'kuisulubisha' miili yetu ya nyama. Ni kwa njia hii tunavyoweza kujifananisha na mauti ya Kristo. Hili ndilo linalotupatia ushindi juu ya dhambi na kutuwezesha kuushiriki uzima wa Kristo pasipo kuwa chini ya vifungu vya maagizo na sheria. Paulo analithibitisha hili anapoandika, *"Katika ungwana huo Kristo alituandika huru; kwa hiyo simameni, wala msinaswe tena chini ya kongwa la utumwa..."* (Wagalatia 5:1).

## Je uhuru unaweza kuwa hatari?

Paulo pia anatuonya kuhusu hatari za uhuru: *"Maana ninyi, ndugu, mliitwa mpate uhuru; lakini uhuru wenu usiwe sababu ya kuufuata mwili…"* (Wagalatia 5:13).

Hata hivyo, wachungaji hawapaswi kuhofia Wakristo kuwa huru kuchagua jinsi wanavyotaka kuyaishi maisha yao. Na la muhimu zaidi hata kuliko hili ni kwamba wanapaswa kuwa makini wasitumie aina hii ya hofu kama kigezo cha kulazimishia kanuni na sheria juu ya Kanisa, na hivyo kuwanyang'anya waumini uhuru walio nao katika Kristo. Cha kusikitisha ni kwamba hii ndiyo hali inayotawala katika makanisa mengi leo.

Hebu niweke jambo moja wazi: si uhuru unaotusababisha tushindwe na tamaa zetu za kimwili. Hata mtu akijiweka chini ya Sheria, ikiwa hataki kumfuata Yesu ataendelea kuishi kwa kuufuata mwili. Lakini ujumbe wa msalaba unapohubiriwa Kanisani, Wakristo wanakuwa huru kabisa kuchagua iwapo watamfuata Kristo au la. Uchaguzi huu na huu utii ndivyo vinavyoleta utofauti. Hili linawawezesha Wakristo kumtumikia Bwana kwa kuitegemea neema yake na sio nguvu zao wenyewe. Ikiwa wataanguka katika dhambi, ni ufunuo wa neema tu utakaowalinda wasianguke katika hukumu. Ufunuo

huu unafungua mlango kwa ajili ya toba, jambo linalowaruhusu kurejea tena na kuendelea na mbio zao.

## Uhuru wa kumpendeza Mungu

Maadam tunauchukua msalaba wetu na kumfuata Yesu, uhuru wetu katika Kristo utatuongoza kumtii Mungu na kukua katika utu uzima rohoni. Katika Kanisa la Kwanza, Wayahudi walioongoka walipata shida kuukubali huu uhuru kwa sababu bado walikuwa wameshikamana sana na Sheria ya Musa na maagizo ya Kilawi. Katika Matendo ya Mitume 10:13-15, tunasoma kwamba hata Mtume Petro mwenyewe alikuwa amefungwa na sheria hizi, alipokataa kula wanyama ambao kwa mujibu wa Torati ya Musa walikuwa najisi. Hata alimhoji Bwana kuhusu jambo hili! Lakini katika Wagalatia 2:11-12 tunaona ya kwamba alifikia kufunguliwa kutokana na utumwa wa Torati, aliposhiriki chakula pamoja na Wayunani waliokuwa wameokoka, ingawa hili ni jambo ambalo halikuruhusiwa kwa Wayahudi chini ya Agano la Kale. Haikuwa rahisi kwake kuiacha Torati pamoja na maagizo yake, lakini ilikuwa ni hatua ya lazima katika kuishi na kumtumikia Bwana katika uhuru.

Kwa namna iyo hiyo, kwa sababu sisi tuko huru mbali na Sheria ya Musa, tunaitwa kuuchukua msalaba wetu kila siku, ikiwa tutataka kutembea katika Roho na si katika mwili. Ni katika kuzifia tamaa zetu za kimwili ndipo tu tutaweza kuishi katika uhuru na kumpendeza Bwana.

## Sura ya XIV

# Msalaba na Uhai wa Kristo Ndani Yetu

Tumeangalia upya msingi wa maisha ya Ukristo: ni Yesu Kristo, naye amesulubiwa. Tumeona ya kwamba mateso, kifo na kufufuka kwake ndicho kiini cha Injili. Ikiwa Wakristo watajifananisha na Kristo katika mateso yake na kifo chake, wataweza kujifananisha na ufufuo wake pia, au kwa maneno mengine, wataubeba uhai wake.

Nabii Isaya alitabiri mateso ya Yesu, kifo chake na kufufuka kwake: *"Lakini Bwana aliridhika kumchubua; amemhuzunisha; utakapofanya nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi, ataona uzao wake, ataishi siku nyingi, na mapenzi ya Bwana yatafanikiwa mkononi mwake..."* (Isaya 53:10). Kufufuka kwake Yesu na kupaa kwake hadi mkono wa kuume wa Baba yake ni matokeo ya maisha yake yasiyo na dhambi, utii wake kamili na kujinyenyekeza kwake katika kuutimiza mpango na mapenzi ya Mungu. *"Alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba. Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno..."* (Wafilipi 2:8-9).

## Kuushiriki uzima wa Kristo

Kama waumini wa Agano Jipya, sehemu muhimu ya maisha yetu ya Ukristo ni kuudhihirisha na kushiriki na wengine uzima wa Yesu. Inabidi turudie kusema ya kwamba hatutaweza kuushiriki uzima wa Kristo ikiwa hatutakuwa tayari kuyashiriki yale yale aliyoyapitia. Kuna gharama ya kulipa: ni kuutoa uhai wetu katika kukubali kuteseka kwa ajili ya Yesu na kuzifia tamaa zetu wenyewe. Huu ndio urahisi na kiini cha maisha ya Ukristo; kiini hasa cha fundisho la Yesu kwa wanafunzi wake, na ndio ujumbe mitume wa kwanza waliolihubiria Kanisa la Kwanza.

Nilimsikia mhubiri mmoja hivi karibuni akitangaza kwenye luninga ya Kikristo ya kwamba angeagiza moto kutoka mbinguni uwateketeze wale wote walio

kinyume naye na kanisa lake. Ni upuuzi wa namna gani huu! Ni wazi kwamba mtu kama huyu hana ufunuo wa injili. Inawezekanaje mtu kama huyu asiye na ufahamu wa moyo wa Bwana aaminiwe maisha ya kundi la Bwana; mtu ambaye, badala ya kuleta *"roho iliyovunjika na kupondeka"*, anauachia mwili wake umtawale? Ni dhahiri kwamba hajui jambo lolote juu ya kujikana nafsi na tamaa zake kwa ajili ya kuudhihirisha uhai wa Kristo. Lakini uelewa huu ni wa muhimu kwa mhubiri zaidi sana kuliko hata Mkristo wa kawaida. Kama Mtume Paulo asemavyo waziwazi, *"Basi hapo mauti hufanya kazi ndani yetu, bali uzima ndani yenu."* (2 Wakorintho 4:12).

Kila Mkristo anapaswa kuamka kutoka katika usingizi na kuacha kukubali kila aina ya mafundisho na mahubiri. Paulo mwenyewe anatuonya, *"Jaribuni mambo yote; lishikeni lililo jema."* (1 Wathesalonike 5:21).

Mwanzoni mwa miaka ya 2000, nilipokuwa nikihubiri katika kongamano moja la wachungaji, nilikutana na mchungaji mmoja kutoka Afrika Mashariki. Alikuwa mzee na alikuwa na kundi kubwa la makanisa chini yake. Alijikuta amekata tamaa kiasi kwamba alifikia uamuzi wa kuacha kila kitu na kustaafu kwa kuyaacha majukumu ya makanisa yake mikononi mwa kizazi kichanga. Ibada zetu zilipokuwa zikiendelea, Bwana alimgusa kwa nguvu ya kipekee na akaelewa maana ya kuyafananisha maisha yake na Kristo. Akafahamu ya kuwa Yesu alikuwa akimwita auchukue msalaba wake na kumfuata, na ya kwamba wakati wa kuiacha huduma yake ulikuwa bado. Akiwa amedhamiria kuuitikia mwito wa Mungu, alijazwa imani mpya na maono mapya kwa ajili ya huduma yake na akaamua kuipokea changamoto, licha ya umri wake. Alisonga mbele na akashuhudia mabadiliko mengi katika maisha yake binafsi na makanisani mwake pia. Alijawa na bidii mpya kwa ajili ya kazi ya Mungu. Kwa miaka mingi baadaye huyu ndugu aliendelea kumtumikia Bwana kwa furaha kubwa na, zaidi ya yote, akiwa na upako mpya kutoka kwa Mungu. Utumishi wake uliaksi uhai wa Kristo kuliko hapo awali.

Kila mtumishi wa kweli wa Mungu je, hatamani kumtumikia Bwana katika kuubeba uhai wake? Hiyo ndiyo huduma halisi ya Roho. Ninakumbuka wakati ambapo mimi mwenyewe nilitumika huku nikiwa nimekauka kiroho, nikiwa sina uhai wa Yesu. Sitaki tena kuirudia hali ile... ya kuhubiri andiko, pasipo huduma ya Roho. Mahubiri yangu yalikuwa si chochote zaidi ya mafundisho ya Biblia ambayo yasingeweza kamwe kujenga kitu katika maisha ya mtu awaye yote.

Pale tu nilipoanza kuelewa maana ya kuenenda katika barabara ya msalaba ndipo nilipoanza kuuhisi uhai wa Kristo na huduma ya Roho vikitenda kazi ndani yangu na kupitia kwangu kwa namna isiyokuwa ya kawaida. Hakuna kitu kinachoweza kulinganishwa na kuuleta uzima wa Kristo katika utumishi wetu kwa Bwana, kwamba tunatia moyo, tunaonya, au kuushiriki ujumbe wa injili. Na hili liko ndani ya uwezo wa kila Mkristo aliye tayari kuuchukua msalaba wake na kumfuata Yesu.

Inapendeza Wakristo wakibarikiwa na kutiwa moyo, si kwa sababu wanajaribu kutumia mbinu na taratibu, bali kwa sababu wanapokea injili safi, rahisi na yenye uhai wa Roho. Ikiwa tunataka kulijenga Kanisa na maisha ya Wakristo, tunahitajika kuwapatia uzima wa Kristo. Elimu ya Biblia peke yake haitoshi. Huduma ya Roho ndiyo inayoleta ufunuo wa injili mioyoni mwa watu. Ndiyo maana ni muhimu sana kukazia kwamba uzima wa Kristo ndani yetu ni matunda ya maisha yetu yaliyotolewa dhahibu kwa kadri tunavyokubali kuyaweka madhabahuni. (Warumi 12:1).

Katika Wakolosai 2:1-3, Paulo anadhihirisha shauku ya moyo wake kwa Wakristo wote: *"...ili wafarijiwe mioyo yao, wakiunganishwa katika upendo, wakapate utajiri wote wa kufahamu kwa hakika, wapate kujua kabisa siri ya Mungu, yaani, Kristo. ambaye ndani yake yeye hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika."*

Ni kwa nini, basi, tufukuzane na vitu vya ulimwengu huu huku tukijua Ukristo wa kweli ni kubeba na kuushiriki uhai wa Kristo? Haileti maana kuwashawishi Wakristo kuitumia imani yao kupata vitu vya dunia hii.

Kinyume chake, imetupasa kushika sana fundisho lenye uzima la Kristo katika kila eneo la maisha yetu, kwa kuifuata roho ya Injili. Hebu tumfuate Yesu ili tuweze kuubeba uzima wake. Katika nyakati ngumu maishani mwetu, tutaweza kuufurahia utumishi wetu kwa Bwana katika ushindi na uhuru, huku tukiingoja thawabu yetu ya mbinguni.

# Wokovu katika Yesu Kristo

Ikiwa kijitabu hiki kimeyagusa maisha yako, tumia muda kidogo kuitafakari mistari michache ifuatayo... Biblia inasema katika Yohana sura ya 3 mstari wa 16, kwamba, *“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.”*

Biblia ni Neno la Mungu na inatufundisha kwamba mtu haokolewi kwa matendo, au dini, bali tu kupitia imani katika dhabihu ya Yesu Kristo ambaye alilipa deni la dhambi zetu msalabani.

Alipokuwa akizungumza na Nikodemo, kuhani wa Kiyahudi, Yesu alimwambia, *“Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.”* Alisema pia, *“Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.”* (Yohana 14:16).

Mtume Yohana analielezea hivi, *“Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake; waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu.”* (Yohana 1:12-13).

Leo, ikiwa hutaki kuendelea kutengwa na Mungu kwa ajili ya dhambi yako lakini unatamani kupatana naye, unaweza kutumia sala ifuatayo kukusaidia kuzungumza na Bwana:

*“Bwana, naja kwa unyenyekevu mbele yako na kutambua kwamba mimi ni mwenye dhambi. Ninaamini ya kwamba Yesu ni Mwanao na ya kwamba alikuja duniani kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zangu ili nipate kusamehewa. Ninaamini pia ya kwamba alifufuka na yuko hai leo. Bwana Yesu, nakuomba unisamehe dhambi zangu, na ninayatoa maisha yangu kwako leo. Ninakupokea kama Bwana na Mwokozi wangu, na asante kwa zawadi ya uzima wa milele.”*

Mungu akubariki!

Ikiwa ungependa kuwasiliana nasi, tutafurahi kukusaidia kumjua Yesu vizuri na kumfuata.

CHURCH TEAM MINISTRIES
INTERNATIONAL

**Wasiliana nasi:**


Kenya +254 719 370 389
Malawi +265 999 94 02 06
Nigeria +234 803 349 4718
South Africa +27 31 765 2927
Tanzania +255 754 827 210
Uganda +256 752 569474
United Kingdom +44 (0) 7922 545867
USA (+1) 800 504 0900
Zimbabwe +263 9 287699

**HEAD OFFICE**
Trianon, Mauritius
+230 403 4500 | info@ctmi.org
**www.ctmi.org**

# Changamoto Ya Msalaba

Wakristo wanaweza wakaamini ya kwamba Biblia ni Neno la Mungu lililovuviwa, wakamkiri Yesu kuwa ni Bwana na Mwokozi na wakatamani kumtumikia kwa moyo. Lakini, je, wanaelewa kikamilifu ya kwamba tumeitwa kuuchukua msalaba wetu kila siku na kumfuata; kuyafananisha maisha yetu na mauti yake, mateso yake na kufufuka kwake, kama vile yeye mwenyewe alivyotuamuru?

Mtume Paulo anazungumzia huku kufananishwa anapoielezea shauku yake binafsi, *"ili nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake; ili nipate kwa njia yo yote kuifikia kiyama ya wafu."* (Wafilipi 3:10).

Tunapolisoma Agano Jipya kwa umakini, tunaona ya kwamba msalaba upo katikati ya kila eneo la maisha ya Ukristo. Msalaba ndio unaotuwezesha kuuitikia wito wa Mungu, na kupata ushindi dhidi ya dhambi. Kwa njia ya msalaba, uweza na neema ya Mungu vinafunuliwa kwetu na kwa njia hii tunalindwa dhidi ya mafundisho ya uongo yanayoweza kuliharibu kanisa.

Hakuna njia bora ya kumjua Kristo kuliko kuishiriki neema yake anapokuwa akiifanya kazi ya kina ndani mwetu, kama mfinyanzi aundapo chombo. Nyakati za kuvunjika, pale tunapokuwa tukizifia nafsi zetu, ndipo tunapokuwa karibu zaidi na yeye na ndipo tunapoijua amani na furaha yake.

Ni wakati muafaka kwa Wakristo wote kuufahamu fika utimilifu wa wito wa Yesu: *"Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate."* (Luka 9:23).

---

*"Injili, na mabadiliko yanayopaswa kufuata utii wetu kwa Kristo zimefafanuliwa kwa uwazi sana katika kitabu hiki. Hatuwezi kufanyika wanafunzi wa kweli wa Yesu ikiwa hatutaelewa au kutamani kukumbatia kile Neno la Mungu linachotuagiza. Asante Mchungaji Miki kwa kuuweka wazi huu ujumbe."*

**Erin Georgiou - Joy! Magazine, Afrika Kusini**

---

Changamoto Ya Msalaba

Miki Hardy

ctmi

CTMI ni mtandao wa Kikristo usio rasmi ulioanzishwa mwaka 2001 na timu ya viongozi kutoka nchi mbalimbali barani Afrika ambao wanaunganishwa na ujumbe wa msalaba na kazi ya Mungu maishani mwao.

Church Team Ministries International | Trianon, Mauritius
(230) 403 4500 | info@ctmi.org | www.ctmi.org

SWAHILI
ISBN 978-99949-941-4-4
9 789994 994144